



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

**MWONGOZO WA
MAADHIMISHO NA
SHEREHE ZA KITAIFA**

JULAI 2011

YALIYOMO

DIBAJI.....	iv - vi
UTANGULIZI.....	1
SURA YA KWANZA: UTARATIBU WA SERIKALI MPYA	
KURINGIA MADARAKANI.....	3
SEHEMU YA KWANZA: MUUNDO NA MAJUKUMU YA KAMATI	4-11
SEHEMU YA PILI: MAANDALIZI	12-19
SEHEMU YA TATU: KIAPO.....	20- 31
SEHEMU YA NNE: TAFRIJA NA DHIFA	32
SURA YA PILI: MAADHIMISHO NA SHEREHE	
ZA TAIFA.....	33
SEHEMU YA KWANZA: ORODHA YA MAADHIMISHO	
NA SHEREHE ZA TAIFA	34- 41
SEHEMU YA PILI: MUUNDO NA MAJUKUMU YA	
KAMATI.	42- 52
SEHEMU YA TATU: VIFAA NA VITENDO MUHIMU	
KATIKA SHEREHE ZA TAIFA	53 - 54
SEHEMU YA NNE: SHEREHE ZA UHURU NA	
JAMHURI	55-71
SEHEMU YA TANO: SHEREHE ZA MUUNGANO	72- 87
SEHEMU YA SITA: KUMBUKUMBU YA MASHUJAA	88 - 98
SEHEMU YA SABA: SHEREHE ZA MAPINDUZI	
ZANZIBAR	99 - 101
SEHEMU YA NANE: SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI (MEI MOSI).....	102 - 109

SEHEMU YA TISA: MAONYESHO YA BIASHARA YA	
KIMATAIFA.....	110 -116
SEHEMU YA KUMI: SIKUKUU YA WAKULIMA (NANENANE).....	117-121
SEHEMU YA KUMI NA MOJA: KUMBUKUMBU YA	
MWALIMU NYERERE NA KILELE CHA MBIO ZA MWENGE	122 -128

SURA YA TATU: MISIBA YA VIONGOZI WA KITAIFA NA VIONGOZI WENGINE	129
SEHEMU YA KWANZA: VIONGOZI AMBAO MISIBA YAO NI YA KITAIFA	130
SEHEMU YA PILI: KAMATI ZA MAZISHI YA VIONGOZI WA KITAIFA	131 -134
SEHEMU YA TATU: MAENEO YA KUZIKIA NA AINA ZA MAZISHI.....	135 - 136
SEHEMU YA NNE: MAZISHI.....	137-141

DIBAJI

Tangu Tanganyika na Zanzibar ziungane Aprili, 1964 na kuundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taifa limekuwa likifanya Maadhimisho na Sherehe na kushughulikia misiba mbalimbali ya Kitaifa.

Maadhimisho hayo ni pamoja na kumbukumbu ya Uhuru na Jamhuri, Mapinduzi ya Zanzibar, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Kumbukumbu ya Mashujaa.

Pamoja na Maadhimisho yaliyoainishwa hapo juu, zipo pia Sherehe za Serikali mpya kuingia madarakani kila baada ya kufanyika Uchaguzi Mkuu. Sherehe hizo zinajumuisha Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na hatimaye Baraza la Mawaziri.

Aidha, katika nyakati tofauti Taifa limepata misiba mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa na kuishughulikia kulingana na maelekezo na mazingira ya wakati huo.

Hata hivyo, pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza matukio hayo, utekelezaji wake ulikuwa hauna Mwongozo rasmi. Kwa hali hiyo, ni dhahiri utekelezaji wa aina hiyo ulikuwa na upungufu wa hapa na pale na hivyo kuathiri ufanisi kwa namna moja au nyingine.

Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika baada ya Sherehe za Serikali ya Awamu ya Nne kuingia Madarakani Desemba, 2005, moja ya mapendekezo ya msingi yaliyotokana na tathmini hiyo ni Serikali kuandaa Mwongozo mahsusi kuhusu Maadhimisho na Sherehe mbalimbali za Taifa utakaoweka taratibu za wazi na endelevu kwa ajili ya kurahisisha rejea na utekelezaji wa shughuli hizo.

Kutokana na maelezo ya hapo juu, Serikali imeandaa Mwongozo kuhusu Maadhimisho, Sherehe na Misiba ya Viongozi wa Kitaifa ambao utatumika katika matukio mbalimbali kama yalivyoainishwa na kufafanuliwa katika Sura na Sehemu mbalimbali za Mwongozo huu. Mwongozo huu umezingatia pia uzoefu uliopatikana katika Sherehe za kuingiza Serikali Mpya Madarakani zilizofanyika Novemba, 2010.

Inawezekana Mwongozo huu ukawa na upungufu wa hapa na pale, hususan wakati wa utekelezaji wake. Upungufu huo utakapojitokeza utazingatiwa, utafanyiwa uchambuzi na marekebisho ipasavyo kwa lengo la kuuboresha. Aidha, Mwongozo utafanyiwa mapitio mara kwa mara ili kuuboresha kulingana na mahitaji na wakati.

Matarajio ya Serikali ni kwamba Ofisi na wahusika walioainishwa katika utekelezaji wa majukumu katika matukio mbalimbali watatekeleza wajibu wao kwa ukamilifu ili kufanikisha malengo yanayokusudiwa. Watumishi wa Serikali na Taasisi zake wanawajibika kuhudhuria Maadhimisho na Sherehe mbalimbali kama sehemu yao ya kazi. Kwa hali hiyo, Watendaji Wakuu wa sehemu za kazi katika Utumishi wa Umma wanatakiwa kusimamia kwa ukamilifu suala hili. Matarajio yangu ni kwamba kutakuwa na ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa majukumu wakati wa matukio mbalimbali ya Kitaifa na hivyo kuongeza ufanisi.

Aidha, Mwongozo huu umeandaliwa kwa kushirikisha wadau kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Baadhi ya Wizara na Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Ofisi ya Rais, Ikulu, Ofisi ya Rais, Usalama wa Taifa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mwisho, wahusika wote katika Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa na katika matukio mengine ya Kitaifa wanatakiwa kusoma na kuelewa Mwongozo huu na kuutekeleza kwa ukamilifu.



MIZENGO P. PINDA, (MB)

Julai, 2011

WAZIRI MKUU

MWONGOZO KUHUSU MAADHIMISHO, SHEREHE NA MISIBA YA VIONGOZI WA KITAIFA

UTANGULIZI

Mwongozo kuhusu Maadhimisho, Sherehe na Misiba ya Kitaifa umeandaliwa kwa lengo la kuweka utaratibu rasmi na wa kudumu wa kufuatwa katika matukio hayo. Mwongozo huu unatoa ufafanuzi wa jinsi ya kuandaa, kuratibu na kusimamia utaratibu wa Serikali mpya kuingia Madarakani; Maadhimisho na Sherehe za Taifa na Misiba ya Viongozi wa Kitaifa na Viongozi wengine.

Sura ya kwanza inahusu utaratibu wa Serikali mpya kuingia Madarakani. Utaratibu huo umegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu Muundo na majukumu ya Kamati zitakazosimamia Serikali mpya kuingia madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu, Sehemu ya pili inahusu maandalizi na taratibu zinazohusu kiapo, Sehemu ya tatu inahusu mahitaji muhimu wakati wa Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri; Itifaki ya Viongozi wanapoingia na kutoka katika eneo la Kiapo; taratibu za kufuatwa katika Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais wanapoingia madarakani kwa mara ya kwanza na kwa mara ya pili, Kiti cha Rais kinapokuwa wazi, Kiti cha Makamu wa Rais kinapokuwa wazi, Kiapo cha Waziri Mkuu na Kiapo cha Mawaziri na sehemu ya nne inahusu tafrija na dhifa zinazohusiana na matukio hayo.

Sura ya Pili inahusu maandalizi na usimamizi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa. Katika Sura hii Mwongozo umeainisha Maadhimisho na Sherehe za Taifa zenye mapumziko na zile zisizo na mapumziko.

Aidha, umewekwa utaratibu wa namna sherehe za kitaifa zitakavyoratibiwa na kusimamiwa iwapo zitaadhimishwa nje ya Dar es Salaam. Mwongozo pia umeainisha Sherehe za Kitaifa zinazosimamiwa moja kwa moja na Serikali, Kamati na vyombo vitakavyohusika na maandalizi, hatua za maandalizi pamoja na vifaa vinavyohitajika katika kufanikisha sherehe hizo. Katika Sura hii pia, Itifaki ya viongozi kuingia, kukaa na kutoka katika maeneo ya maadhimisho ya sherehe mbalimbali imefafanuliwa.

Sura ya Tatu inahusu utaratibu wa namna ya kushughulikia Misiba na Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa. Kulingana na Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa Na. 1/2006, utaratibu huu unawahusu viongozi waliopo madarakani na wale waliostaafu kama ilivyoainishwa na Sheria hiyo ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu umefafanua Viongozi wanaostahili mazishi ya kitaifa, Kamati iliyoundwa kisheria na majukumu yake katika kusimamia misiba ya kitaifa, maeneo maalum ya kuzikia Viongozi wa Kitaifa na aina za mazishi, utaratibu wa kufuatwa unapotokea msiba wa Kitaifa, utoaji wa heshima za mwisho na upatikanaji wa fedha na mahitaji mengine kwa ajili ya kufanikisha mazishi ya Kitaifa.

SURA YA KWANZA

UTARATIBU WA SERIKALI MPYA KUIINGIA MADARAKANI

Sura hii inaeleza utaratibu wa Serikali mpya kuingia Madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Utaratibu huu unaweka na kufafanua Muundo na Majukumu ya Kamati mbalimbali za Maandalizi na kuainisha mahitaji muhimu kwa ajili ya shughuli ya Serikali mpya kuingia madarakani.

Utaratibu ulioainishwa umezingatia matukio muhimu ya kuiwezesha Serikali mpya kuingia madarakani ambayo ni pamoja na: Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri na Tafrija kwa wageni mbalimbali.

SEHEMU YA KWANZA

MUUNDO NA MAJUKUMU YA KAMATI

Kutakuwa na Kamati mbili za Maandalizi ya Serikali mpya kuingia Madarakani. Kamati ya Watendaji Wakuu na Kamati ya Wataalam.

(a) KAMATI YA WATENDAJI WAKUU (EXECUTIVE COMMITTEE)

Kamati ya Watendaji Wakuu itakuwa na Wajumbe wafuatao:

- (i) Katibu Mkuu Kiongozi - Mwenyekiti
- (ii) Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Makamu
Mwenyekiti
- (iii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana
ya Katiba na Sheria - Mjumbe
- (iv) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mjumbe
- (v) Katibu Mkuu, Ikulu - Mjumbe
- (vi) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana
ya Fedha na Uchumi - Mjumbe
- (vii) Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mjumbe
- (viii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa
Kimataifa - Mjumbe
- (ix) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana
ya Habari, Utamaduni na Michezo - Mjumbe
- (x) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana
ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Mjumbe
- (xi) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya
Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mjumbe

- | | |
|--|----------|
| (xii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Miundombinu | - Mjumbe |
| (xiii) Msajili wa Mahakama ya Rufani | - Mjumbe |
| (xiv) Katibu wa Bunge | - Mjumbe |
| (xv) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali | - Mjumbe |
| (xvi) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi | - Mjumbe |
| (xvii) Inspekta Jenerali wa Polisi | - Mjumbe |
| (xviii) Kamishna Mkuu wa Magereza | - Mjumbe |
| (xix) Mkurugenzi Mkuu, Idara ya Usalama wa Taifa | - Mjumbe |
| (xx) Mganga Mkuu wa Serikali | - Mjumbe |
| (xxi) Mkurugenzi wa Huduma za Ikulu | - Katibu |

Majukumu ya Kamati ya Watendaji Wakuu

Majukumu ya Kamati ya Watendaji Wakuu ni pamoja na kutoa maelekezo kwa Kamati ya Wataalam, kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za Kamati ya Wataalam zinazohusika na Serikali mpya kuingia madarakani, ikiwa ni pamoja na Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri.

(b) KAMATI YA WATAALAM (TECHNICAL COMMITTEE)

Kamati ya Wataalam (Technical Committee) itakuwa na wajumbe wafuatao:

- (i) Katibu Mkuu, Ikulu - Mwenyekiti
- (ii) Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mjumbe
- (iii) Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mjumbe
- (iv) Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mjumbe
- (v) Naibu Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Fedha na Uchumi - Mjumbe
- (vi) Mkurugenzi, Idara ya Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais - Mjumbe
- (vii) Mkurugenzi, Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mjumbe
- (viii) Mkuu wa Itifaki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mjumbe
- (ix) Karani wa Baraza la Mawaziri, Ikulu - Mjumbe
- (x) Mnikulu, Ofisi ya Rais, Ikulu - Mjumbe
- (xi) Mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi - Mjumbe
- (xii) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mjumbe
- (xiii) Mwakilishi kutoka Jeshi la Magereza - Mjumbe
- (xiv) Mwakilishi kutoka Idara ya Usalama wa Taifa - Mjumbe
- (xv) Mwakilishi kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania - Mjumbe
- (xvi) Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) - Mjumbe
- (xvii) Msajili wa Mahakama Kuu - Mjumbe
- (xviii) Mwakilishi wa Katibu wa Bunge - Mjumbe

- (xix) Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Serikali - Mjumbe
- (xx) Mkurugenzi wa Huduma za Ikulu - Katibu

WAJUMBE WA KUALIKWA (CO-OPTED)

Kamati inaweza kualika wajumbe wafuatao au wengine kama itakavyoona inafaa:

- (i) Katibu Tawala wa Mkoa (Dar es Salaam/Dodoma)
- (ii) Kamishna wa Uhamiaji
- (iii) Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji
- (iv) Meneja wa Uwanja wa Uhuru
- (v) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege
- (vi) Mkurugenzi wa Jiji
- (vii) Mtendaji Mkuu wa TANROADS
- (viii) Mkurugenzi, Idara ya Utamaduni

Majukumu ya Kamati ya Wataalam

Majukumu ya Kamati ya Wataalam ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kupokea na kutekeleza maelekezo kutoka katika Kamati ya Watendaji Wakuu.
- (ii) Kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za kamati ndogo za Itifaki, Mialiko na Sherehe, Ulinzi, Usalama na Gwaride la Heshima na Viapo.
- (iii) Kutoa taarifa za utekelezaji kwa Kamati ya Watendaji Wakuu.

KAMATI NDOGO ZA KAMATI YA WATAALAM

Kutakuwa na Kamati ndogo tatu za wataalam ambazo wajumbe wake watateuliwa kutoka kwenye Kamati ya Wataalam. Wajumbe wa Kamati hizo, na majukumu yake ni kama ifuatavyo:

(i) Kamati Ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe

Wajumbe:

- Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mwenyekiti
- Mkurugenzi Maadhimisho na Sherehe za Taifa
- Mwakilishi TISS
- Mkuu wa Itifaki
- Mnikulu
- Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO)
- Msajili wa Mahakama ya Rufani
- Mwakilishi wa Katibu wa Bunge

MAJUKUMU

Majukumu ya Kamati ni kama ifuatavyo:

- Kuandaa orodha ya waalikwa wa ndani na nje ya nchi.
- Kuandaa kadi za mialiko.
- Kuandaa ratiba ya uapishaji.
- Kupanga taratibu za kuingia na kukaa katika maeneo ya matukio.
- Kusimamia ujenzi wa majukwaa yatakayotumika wakati wa kuapishwa Rais na Makamu wa Rais, na Waziri Mkuu.
- Kuhakikisha uwepo wa vifaa muhimu wakati wa uapisho kama vile vipaza sauti, mahema, mazulia, viti, na majukwaa mbalimbali.
- Kuandaa taratibu za usafiri kwa waalikwa kutoka ndani na nje ya nchi.

- Kuandaa dhifa na tafrija.
- Kuandaa vikundi vya kutoa burudani kama ngoma, muziki wa dansi, matarumbeta na kwaya.
- Kusimamia mapambo katika maeneo yote ya matukio kama vile maua, bendera, mabango na bendera ndogo za Taifa za kupeperusha.
- Kuandaa huduma za afya katika maeneo mbalimbali ya matukio kama vile magari ya wagonjwa, madaktari na wauguzi wa huduma ya kwanza.
- Kurekodi na kutunza kumbukumbu za matukio yote ya sherehe na viapo.
- Kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana katika maeneo ya matukio kama vile maji, umeme, vyoo, jenereta na magari ya zimamoto.
- Kuratibu na kusimamia waandishi wa habari na wapiga picha.
- Kuhamasisha wananchi kuhudhuria katika sherehe za uapishaji.
- Kuandaa na kusimamia eneo la uapisho wa Waziri Mkuu Ikulu.
- Kuandaa na kusimamia eneo la Uapisho wa Mawaziri, Ikulu.
- Kuwasiliana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu tarehe ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais.

(ii) Kamati Ndogo ya Ulinzi, Usalama na Gwaride la Heshima

Wajumbe:

- Naibu Katibu Mkuu Hazina - Mwenyekiti
- Mwakilishi JWTZ
- Mwakilishi TISS
- Mwakilishi Polisi
- Mwakilishi Magereza

MAJUKUMU

Majukumu ya kamati ni kama ifuatavyo:-

- Kuratibu mipango na kusimamia Ulinzi na Usalama katika maeneo yote ya matukio.
- Kuratibu maandalizi ya Gwaride la Heshima.
- Kuhakikisha kuwa uwanja wa maadhimisho uko katika hali nzuri.
- Kuhakikisha kuwa barabara zitakazotumiwa na viongozi kwenda Uwanja wa Maadhimisho zipo katika hali nzuri.
- Kuandaa gwaride la mapokezi ya Viongozi Wakuu wa Nchi walioalikwa.
- Kuratibu na kufanikisha usafiri wa viongozi na wageni siku ya Kiapo cha Rais.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama katika maeneo watakayofikia wageni kutoka nchi za nje.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama katika maegesho ya magari.
- Kuratibu na kusimamia Ulinzi na Usalama katika eneo la kutangazia matokeo ya Uchaguzi wa Rais.

(iii) Kamati Ndogo ya Viapo

Wajumbe:

- Naibu Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mwenyekiti
- Karani wa Baraza la Mawaziri
- Mkurugenzi Idara ya Muungano
- Mwakilishi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
- Msajili Mahakama Kuu.

MAJUKUMU

Majukumu ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

- Kuandaa Viapo vya Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri.
- Kuhakikisha kwamba vifaa vya kuapishia vinapatikana. Vifaa hivyo ni:-
 - Biblia, Quran na Katiba ya nchi
 - Ngao, Mkuki na Kigoda
 - “Flaps” za mezani na za kushikia kiapo
- Kushirikiana na Kamati Ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe na Kamati ya Ulinzi, Usalama na Gwaride la Heshima katika Ujenzi wa Jukwaa la Kiapo.
- Kuwaandaa Wazee wa kumkabidhi Rais Alama za Mamlaka (Symbols of Power).
- Kuhakikisha upatikanaji wa mavazi yatakayovaliwa na wazee watakaomkabidhi Rais Alama za Mamlaka.
- Kuratibu na kusimamia mpangilio wa kukaa katika Jukwaa la Kiapo.

SEHEMU YA PILI

MAANDALIZI

Sherehe za Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wanapoingia madarakani zinafanyika baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi Mkuu. Hatua za maandalizi ya sherehe za Kiapo ni kama ifuatavyo:-

(a) TAARIFA NA VIKAO

- (i) Mwenyekiti wa Kamati ya Watendaji Wakuu (Executive Committee) ataitisha kikao cha kwanza cha maandalizi mwezi Januari ya mwaka wa Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya kuandaa bajeti ya shughuli ya Serikali mpya kuingia madarakani. Aidha, miezi miwili kabla ya Uchaguzi Mkuu ataitisha mkutano wa kuanza rasmi maandalizi ya shughuli ya Serikali mpya kuingia madarakani. Baada ya Serikali mpya kuingia madarakani kutakuwa na kikao cha tathmini.

- (ii) Kutakuwa na vikao sita vya Kamati ya Watendaji Wakuu kwa ajili ya maandalizi ya Serikali mpya kuingia madarakani kama ifuatavyo:-
 - Kikao cha kwanza kitakuwa ni cha Kamati ya Watendaji Wakuu kutoa maelekezo na maagizo kwa Kamati ya Wataalam.
 - Kikao cha pili ni cha kupokea makadirio ya gharama za sherehe kutoka katika Kamati ya Wataalam.
 - Kikao cha tatu ni cha kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu kutoka katika Kamati ya Wataalam.

- Kikao cha nne ni cha kupokea taarifa ya mwisho ya maandalizi kwa kupitia utekelezaji wa masuala yaliyoelekezwa katika Kikao cha kwanza, cha pili na cha tatu.
 - Kikao cha tano ni mazoezi kwa vitendo katika eneo la tukio. Kikao hiki kitahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na jopo la kiapo, jopo la majaji, washereheshaji, kamati ya maandalizi, waandishi wa habari na wapiga picha.
 - Kikao cha tathmini baada ya Serikali mpya kuingia madarakani kitafanyika ndani ya mwezi mmoja baada ya Baraza la Mawaziri kuapishwa.
- (iii) Kutakuwa na vikao vitano vya Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kutekeleza maagizo mbalimbali yatakayotolewa na Kamati ya Watendaji Wakuu (Executive Committee). Aidha, kutakuwa na kikao cha sita cha tathmini baada ya Serikali mpya kuingia madarakani.

(b) MAHITAJI

Utekelezaji wa shughuli za Serikali mpya kuingia madarakani zitafanyika uwanjani, kwa sasa shughuli hizo zinafanyika katika uwanja wa Uhuru ambao sura yake ni kama inavyoonekana katika **ukurasa wa 26 wa kitabu cha pili kinachoonesha michoro na vitendo uwanjani**. Pamoja na mambo mengine vifaa vifuatavyo vitahitajika:-

(i) Vifaa Maalum vya Kiapo

- Meza ya kiapo
- Viti mahsusi kwa ajili ya Rais, Makamu wa Rais, Jaji Mkuu n.k.
- Biblia, Quran na Katiba
- Flaps za Mezani na kushikia kiapo
- Mkuki
- Ngao
- Kigoda
- Kalamu
- Hati za viapo
- Vifaa vya kukaushia wino

(ii) Jukwaa la Kiapo

Kutakuwa na Jukwaa la Kiapo ambalo litajengwa Uwanja wa Uhuru mita 20 kutoka mstari wa katikati ya Uwanja kuelekea upande wa Kaskazini. Jukwaa hilo litajengwa mita mbili (2) kutoka ukingo wa Uwanja. Kamati ya Itifaki, Mialiko na Sherehe kwa kushirikana na kamati ya viapo zitaratibu upatikanaji wa vifaa hivyo.

(iii) Mahema

Kamati ya viapo itaratibu ujenzi wa Jukwaa la Kiapo. Kutakuwa na mahema ya ukubwa mbalimbali ya kutosha shughuli zote katika uwanja wa kiapo kama vile “brass band”, Huduma ya kwanza, vikundi vya ngoma na bendi za muziki wa dansi. Uwekaji wa mahema utaratibiwa na Kamati Ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe.

(iv) Viti

Vitaandaliwa viti vya kutosha kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa katika eneo la Jukwaa Kuu. Aidha, kutakuwa na viti vya kutosha kwa ajili ya wananchi katika eneo la Uapisho.

Uwekaji wa viti hivyo utaratibiwa na Kamati ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe.

(v) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja wa uapisho kwa ajili ya wageni na wananchi kufuatilia matangazo na matukio. Kamati ya Itifaki, mialiko na Sherehe itaratibu upatikanaji wa vipaza sauti hivyo.

(vi) Jukwaa la Viongozi wa Kitaifa

Kamati ya Itifaki, Mialiko na Sherehe itaandaa jukwaa la Viongozi wa Kitaifa mahali ambapo sherehe zitafanyika.

(vii) Mazulia Mekundu

Kamati ya Itifaki, Mialiko na Sherehe itaandaa mazulia mekundu sehemu watakayopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa.

(viii) Mapambo

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa mapambo ya kutosha kwa ajili ya shughuli ya Uapisho, kama vile maua, bendera, mabango na bendera ndogo za kupeperusha.

(i) Luninga kubwa ya Nje

Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaratibu upatikanaji wa luninga kubwa ya nje kwa ajili ya waalikwa na wananchi kufuatilia matukio nje na ndani ya uwanja.

(ii) Majukwaa

Kutakuwa na majukwaa kwa ajili ya waandishi wa habari na wapiga picha ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Jukumu hili litaratibiwa na Kamati ya Itifaki, Mialiko na sherehe kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi, Usalama na Gwaride.

(iii) Jukwaa dogo la kupokelea Heshima (Saluting Dais)

Kutakuwa na jukwaa dogo la kupokelea heshima kwa ajili ya Rais litakaloandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

(xii) Magari

Kutakuwa na magari yenye hadhi kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa, Wakuu wa nchi waalikwa na Watendaji Wakuu yatakayowasafirisha kutoka sehemu ya mkusanyiko itakayokubalika hadi Uwanja wa Uhuru na kuwarudisha mara baada ya sherehe kuisha. Magari hayo yatakaguliwa na vyombo vya ulinzi na usalama kabla ya kutumika.

(xiii) Vitambulisho

Kutakuwa na vitambulisho vya wajumbe wa Kamati ya Maandalizi vyenye picha na majina vitakavyotumika katika sherehe ya Uapisho. Vitambulisho vitaandaliwa na kuratibiwa na Idara ya Usalama wa Taifa. Waandishi wa Habari wataingia katika sherehe kwa kutumia vitambulisho maalum vitakavyotolewa na Idara ya Usalama wa Taifa.

(xiv) Jenereta

Kamati ya Itifaki, Mialiko na Sherehe itaratibu upatikani wa jenereta uwanjani kwa ajili ya dharura ya umeme kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Jenereta litakuwepo uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe na litakaguliwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

(xv) Bendera

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaratibu upatikanaji wa bendera.

Bendera zitakazopeperushwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Bendera ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

(c) RATIBA

Kamati ya Itifaki Mialiko na Sherehe itandaa rasimu ya Ratiba

(i) Ratiba itazingatia yafuatayo:

- Jina na mahali pa tukio
- Matukio na muda
- Wahusika

(ii) Rasimu ya ratiba itakamilishwa mwezi mmoja kabla ya siku ya kiapo na kuwasilishwa katika Kamati ya Watendaji Wakuu (Executive Committee) kwa ajili ya kuipitia na hatua zaidi.

(d) BARUA NA KADI ZA MIALIKO

(i) Barua za Mialiko

Barua za mialiko zitatayarishwa kwa ajili ya makundi yafuatayo:-

- Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu
- Viongozi kutoka nje ya nchi
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Jaji Mkuu wa Zanzibar waliopo madarakani na wastaafu.
- Viongozi wa Vyama vya Siasa Ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu)
- Viongozi wa Dini(BAKWATA, CCT na TEC,)
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Wageni Maalum kama itakavyoelekezwa na Kamati ya Watendaji Wakuu.

(ii) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitatayarishwa kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Watakaopewa kadi za mialiko ni Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Mabalazi, Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea na Wakurugenzi wa Wizara za Serikali, Viongozi wa Mkoa na Wawakilishi wa Wazee wa Mkoa mahali sherehe zinapofanyika.

Idara ya Sherehe na Maadhimisho Zanzibar itawasilisha orodha ya waalikwa kutoka Zanzibar kwa Kamati ya Maandalizi ili waandaliwe mialiko.

SEHEMU YA TATU

KIAPO

Mtiririko wa vitendo vya Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri utakuwa na utaratibu kulingana na tukio lenyewe. Kutokana na hali hiyo, sehemu hii inafanua utaratibu wa kuwaapisha Rais na Makamu wa Rais wanapoingia madarakani kwa mara ya kwanza, Rais na Makamu wa Rais wanapoingia madarakani mara ya pili, Kiti cha Rais kinapokuwa wazi na Kiti cha Makamu wa Rais kinapokuwa wazi. Aidha, Kiapo cha Waziri Mkuu na Kiapo cha Mawaziri vimewekewa utaratibu na kufafanuliwa.

(a) RAIS NA MAKAMU WA RAIS WANAPOINGIA MADARAKANI KWA MARA YA KWANZA

Utaratibu wa Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais wanapoingia madarakani kwa mara ya kwanza utakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Viongozi wa Kitaifa waliopo Madarakani, Wastaafu pamoja na Viongozi wa Kimataifa watakapoingia Uwanjani watapokelewa na Mkuu wa Mkoa. Kiongozi atakayepokea wageni hao atavaa vazi rasmi (suti nyeusi). Kwa mwanaume suti itavaliwa pamoja na shati jeupe na tai nyekundu.
- (ii) Itifaki ya viongozi kuingia uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-

- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais Wastaafu wa Zanzibar
- Makamu wa Rais wastaafu
- Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Rais anayemaliza muda wake
- Wakuu wa Nchi waalikwa
- Rais anayemaliza muda wake.

(iii) Mara baada ya Wakuu wa Nchi walioalikwa kuingia uwanjani, kutakuwa na maandamano ya Jopo la Kiapo kuelekea katika eneo la Jukwaa la Kiapo.

- Jaji Mkuu
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Viongozi watatu (3) wa madhehebu ya dini
- Wazee wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar
- Karani wa Baraza la Mawaziri
- Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi

- Jopo la Majaji
 - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
 - Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
- (iv) Makamu wa Rais anayeondoka madarakani kuingia uwanjani na kuelekea katika Jukwaa la Kiapo.
- (v) Rais anayeondoka madarakani kuingia uwanjani na:
- Kupokea salamu ya heshima na mizinga 21 kupigwa.
 - Gwaride kuunda umbo la **Omega**.
 - Kukagua Gwaride.
 - Kurejea kwenye Jukwaa dogo la kupokelea heshima
 - Bendera ya Rais kuteremshwa na wimbo wa Taifa kupigwa.
 - Kuelekea kwenye Jukwaa la Kiapo.
- (vi) Rais Mteule na Makamu wa Rais Mteule kuelekea kwenye Jukwaa la Kiapo.
- (vii) Rais Mteule kuapishwa na kukabidhiwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu.
- (viii) Makamu wa Rais Mteule kuapishwa na kukabidhiwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu.
- (ix) Rais kuketi kwenye kiti cha jadi (kigoda) na kukabidhiwa Ngao na Mkuki na wazee.
- (x) Rais kupongezana na Rais anayeondoka madarakani.
- (xi) Makamu wa Rais kupongezana na Makamu wa Rais anayeondoka madarakani.
- (xii) Rais anayeondoka madarakani kumpisha kiti Rais, na kuelekea katika sehemu iliyotengwa kwa ajili yake katika jukwaa la kiapo.
- (xiii) Mpambe na Walinzi wa Rais kuhamia kwa Rais aliyeingia madarakani.
- (xiv) Makamu wa Rais anayeondoka madarakani kumpisha

- kiti Makamu wa Rais, na kuelekea katika sehemu iliyotengwa kwa ajili yake katika jukwaa la kiapo.
- (xv) Dua na sala kusomwa na Viongozi wa dini (BAKWATA, CCT, TEC).
- (xvi) Rais na Makamu wa Rais aliyeondoka madarakani, Makamu wa Rais, Jaji Mkuu, Spika na Katibu Mkuu Kiongozi kuelekea katika Jukwaa Kuu.
- (xvii) Rais kuelekea katika Jukwaa la heshima na kupokea salamu ya heshima:
- Salamu ya Rais.
 - Wimbo wa Taifa na Mizinga 21 kupigwa na bendera ya Rais kupandishwa.
 - Gwaride kuunda umbo la **Alpha**.
 - Rais kukagua Gwaride. Baada ya ukaguzi Rais kurejea jukwaa la heshima.
 - Gwaride kurudi katika safu ya kawaida.
 - Salamu ya Rais na wimbo wa Taifa kupigwa.
 - Gwaride kusonga mbele kwa heshima.
 - Gwaride kutoa Heshima ya Utii kwa Rais.
 - Gwaride kutoka Uwanjani.
 - “Military Band” kurejea Uwanjani kumtoa Rais.
- (xviii) Rais kurejea katika Jukwaa Kuu na kutoa hotuba.
- (xix) Endapo Rais hatatoa hotuba gwaride litabaki uwanjani hadi Rais na Viongozi wengine watakapoondoka.
- Itifaki ya kuondoka Uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
 - Rais aliyekabidhi madaraka
 - Wakuu wa nchi waalikwa
 - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
 - Makamu wa Rais aliyeondoka Madarakani
 - Rais wa Zanzibar

- Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais Wastaafu wa Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu, Zanzibar
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Jopo la Majaji.

**(b) RAIS NA MAKAMU WA RAIS
WANAPOINGIA MADARAKANI KWA
MARA YA PILI**

Rais aliyepo madarakani na Makamu wake wanapoingia madarakani kwa mara ya pili, utaratibu wa kiapo utakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Viongozi wa Kitaifa waliopo Madarakani, wastaafu pamoja na Viongozi wa Kimataifa watakapoingia Uwanjani watapokelewa na Mkuu wa Mkoa. Kiongozi huyo atakayepokea wageni hao atavaa suti nyeusi. Kwa Mwanaume suti itavaliwa pamoja na shati jeupe na tai nyekundu.

(ii) Itifaki ya viongozi kuingia uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-

- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu wastaafu
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais Wastaafu wa Zanzibar
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Wakuu wa Nchi waalikwa

(iii) Mara baada ya Wakuu wa Nchi walioalikwa kuingia uwanjani, kutakuwa na maandamano ya Jopo la Kiapo. Jopo hilo litajumuisha wafuatao:-

- Jaji Mkuu
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Katibu Mkuu Kiongozi.
- Viongozi watatu (3) wa madhehebu ya dini. (BAKWATA, CCT na TEC)
- Wazee wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar.
- Karani wa Baraza la Mawaziri.

- Jopo la Majaji.
 - Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
 - Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
- (iv) Makamu wa Rais kuingia uwanjani na kuelekea katika Jukwaa la Kiapo.
- (v) Rais kuingia uwanjani na:-
- Kupokea salamu ya heshima, Wimbo wa Taifa kupigwa na Bendera ya Rais kuteremshwa (Rais hatakagua Gwaride).
 - Rais kuelekea kwenye Jukwaa la Kiapo.
- (vi) Rais Mteule kuapishwa na kukabidhiwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu.
- (vii) Makamu wa Rais Mteule kuapishwa na kukabidhiwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu.
- (viii) Makamu wa Rais kuelekea katika sehemu iliyotengwa kwa ajili yake katika Jukwaa la kiapo.
- (ix) Rais kuketi kwenye kiti cha jadi (kigoda) na kukabidhiwa Ngao na Mkuki na wazee.
- (x) Rais kuelekea katika sehemu iliyotengwa kwa ajili yake katika Jukwaa la Kiapo.
- (xi) Dua na Sala kusomwa na Viongozi wa dini BAKWATA, CCT, TEC).
- (xii) Rais kuelekea katika Jukwaa dogo na kupokea Salamu ya Heshima:
- Salamu ya Rais.
 - Wimbo wa Taifa na Mizinga 21 kupigwa na bendera ya Rais kupandishwa.
 - Gwaride litaunda Umbo la “Alpha”.
 - Rais kukagua gwaride likiwa limetoa heshima (Present Arms) na baada ya ukaguzi atarejea kwenye “Saluting Dias”.

- Gwaride kurejea katika muundo wake wa awali “Column Formation”
- Gwaride kusonga mbele kwa heshima na kutoa heshima ya utii kwa Rais.
- Gwaride kutoka Uwanjani.
- “Military band” kurejea Uwanjani kumtoa Rais.

(xiii) Rais kwenda katika Jukwaa Kuu na kutoa hotuba.

- Iwapo Rais hatatoa hotuba, gwaride litabaki Uwanjani na kutoka baada ya Rais na Viongozi wengine kuondoka.

(xiv) Itifaki ya kuondoka uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Wakuu wa nchi waalikwa
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Zanzibar
- Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wastaafu
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wastaafu
- Rais wa Zanzibar Wastaafu
- Waziri Mkuu
- Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Mawaziri Viongozi Wastaafu
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Jopo la Majaji.

Sehemu hii isomwe sambamba na Kitabu cha Pili cha michoro kwa vitendo Uk. 65 – 101

(c) KITI CHA RAIS KINAPOKUWA WAZI

Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na masharti ya ibara ya 37(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utaratibu wa Kiapo cha Makamu wa Rais kuwa Rais utakuwa kama ifuatavyo:-

- Kiapo kitafanyika katika Viwanja vya Ikulu
 - Kiapo hakitakuwa na gwaride
 - Kutakuwa na “Brass Band” ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania/Jeshi la Polisi ambayo itapiga Wimbo wa Taifa.
 - Kikundi cha “fanfare” kitapiga baada ya kiapo kukamilika.
- (i) Itifaki ya kuingia katika Viwanja vya Ikulu itakuwa kama ifuatavyo:-
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
 - Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
 - Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
 - Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
 - Mawaziri Wakuu Wastaafu
 - Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
 - Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
 - Marais Wastaafu wa Zanzibar
 - Makamu wa Rais Wastaafu
 - Marais Waastafu
 - Waziri Mkuu
 - Rais wa Zanzibar.

(ii) Itifaki ya kuondoka katika Viwanja vya Ikulu itakuwa kama ifuatavyo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais Wastaafu
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais Wastaafu wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Zanzibar.

(d) KITI CHA MAKAMU WA RAIS KINAPOKUWA WAZI

Endapo Kiti cha Makamu wa Rais kitakuwa wazi kutokana na masharti ya ibara ya 37(5) au ibara ya 50(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kiapo cha Makamu wa Rais Mteule kitakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Makamu wa Rais Mteule ataapishwa na Jaji Mkuu katika viwanja vya Ikulu.
- (ii) Kiapo hakitakuwa na Gwaride.
- (iii) Kutakuwa na “brass band” ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania/Jeshi la Polisi ambayo itapiga wimbo wa taifa.
- (iv) Kikundi cha “fanfare” kitapiga baada ya kitendo cha kuapishwa kukamilika.

(e) KIAPO CHA WAZIRI MKUU

- (i) Waziri Mkuu Mteule ataapishwa na Rais katika viwanja vya Ikulu.
- (ii) Sherehe za Kiapo cha Waziri Mkuu hazitakuwa na gwaride.
- (iii) Kutakuwa na kikundi cha “fanfare” ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania/Jeshi la Polisi ambacho kitapiga “fanfare”.
- (iv) Waalikwa watapewa kadi za mialiko zitakazoandaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.
- (v) Pamoja na Waalikwa wengine, Waalikwa kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama watapatiwa kadi za mialiko kwa idadi ifuatavyo:-
 - JWTZ nafasi - 6
 - Polisi nafasi - 5
 - Magereza nafasi - 6
 - Zimamoto na Uokoaji nafasi - 4

(f) KIAPO CHA MAWAZIRI

- (i) Mawaziri wataapishwa katika viwanja vya Ikulu. Jukwaa la kuapishia litakuwa mita 15 kutoka eneo watakapokaa Waapishwaji.
- (ii) Mawaziri watakaoapishwa watavaa suti nyeusi. Kwa Mawaziri wanaume suti itavaliwa pamoja na shati jeupe na tai nyekundu.

- (iii) Sherehe za Kiapo cha Mawaziri hazitakuwa na gwaride.
- (iv) Kutakuwa na kikundi cha “fanfare” ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania/Jeshi la Polisi ambacho kitapiga “fanfare”.
- (v) Pamoja na Waalikwa wengine, Waalikwa kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama watapatiwa kadi za mialiko kwa idadi ifuatavyo:-
 - JWTZ nafasi - 6
 - Polisi nafasi - 5
 - Magereza nafasi - 6
 - Zimamoto na Uokoaji nafasi – 4

SEHEMU YA NNE

TAFRIJA NA DHIFA

Wakati wa Kiapo cha Rais na Makamu wa Rais, kutakuwa na tafrija na/au dhifa kwa madhumuni mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (a) Itaandaliwa tafrija au chakula cha usiku siku moja kabla ya kiapo cha Rais Mteule kwa ajili ya Rais anayemaliza muda wake kuagana na Viongozi wa nchi za nje watakaohudhuria katika Sherehe za Kiapo.
- (b) Siku ya Kiapo kitaandaliwa chakula cha mchana kwa ajili ya Rais na Viongozi wa nchi za nje waliohudhuria Sherehe za kiapo.
- (c) Siku ya Kiapo, usiku itaandaliwa dhifa au tafrija Ikulu kwa ajili ya Rais kupongezana na viongozi mbalimbali.

Waalikwa watapewa kadi za Mialiko zitakazoandaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho ya Taifa.

SURA YA PILI

MAADHIMISHO NA SHEREHE ZA KITAIFA

Sura hii inaainisha Sherehe za Taifa zinazosimamiwa moja kwa moja na Serikali, vyombo vinavyosimamia maandalizi ya Sherehe, hatua za maandalizi ya Sherehe na vifaa vinavyohitajika katika kufanikisha Sherehe. Sura hii inatoa maelekezo ya jinsi ya kuandaa Maadhimisho na Sherehe mbalimbali za Taifa.

Aidha, umetolewa ufafanuzi wa jinsi Sherehe za Taifa zitakavyoratibiwa na kusimamiwa iwapo zitafanyika nje ya Dar es Salaam. Utaratibu umefafanua majukumu ya Kamati zinazohusika katika kusimamia maadhimisho na Sherehe za Taifa katika ngazi mbalimbali. ***(Sura hii isomwe sambamba na Kitabu cha pili cha michoro ya vitendo kuanzia Uk. 1 hadi uk.29)***

SEHEMU YA KWANZA

ORODHA YA MAADHIMISHO NA SHEREHE ZA KITAIFA

Maadhimisho na Sherehe za Taifa ni kama ifuatavyo:-

(a) Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa zenye Mapumziko (National Public Holidays)

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/SHEREHE
1.	1 Januari	Mwaka Mpya (New Year)
2.	12 Januari	Mapinduzi ya Zanzibar
3.	Machi - Itategemea Kuandama kwa mwezi	Maulid
4.	7 Aprili	Kumbukumbu ya Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume
5.	Kwa mujibu wa kalenda	Ijumaa Kuu
6.	Kwa mujibu wa kalenda	Jumatatu ya Pasaka
7.	26 Aprili	Muungano wa Tanganyika na Zanzibar
8.	1 Mei	Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi)
9.	7 Julai	Kilele cha Maonesho ya Biashara ya Kimataifa(SabaSaba)
10.	8 Agosti	Siku ya Wakulima(NaneNane)
11.	Itategemea kuandama kwa mwezi	Eid El-Fitri

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/SHEREHE
12.	14 Oktoba	Kumbukumbu ya Mwalimu J.K. Nyerere na kilele cha Mbio za Mwenge
13.	Itategemea kuandama kwa mwezi	Eid El-Hajj
14.	9 Desemba	Uhuru na Jamhuri
15.	25 Desemba	Kuadhimisha Kuzaliwa kwa Kristo
16.	26 Desemba	Siku ya Kupeana Zawadi

(b) Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa zisizo na mapumziko

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
1.	01 Januari	Siku ya Upandaji Miti	Wizara yenye dhamana ya Maliasili
2	29 Januari	Siku ya Ukoma	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
3	02 Februari	Siku ya ardhi-oevu (<i>Wetlands Day</i>)	Wizara yenye dhamana ya Utalii
4	27 Februari	Siku ya Utalii	Wizara yenye dhamana ya Utalii
5	08 Machi	Siku ya Wanawake Duniani	Wizara yenye dhamana ya Jinsia
6	16 Machi	Siku ya Maji Duniani	Wizara yenye dhamana ya Maji

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
7	23 Machi	Siku ya Hali ya Hewa	Wizara yenye dhamana na Uchukuzi
8	24 Machi	Siku ya Kifua Kikuu	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
10	27 Aprili	Malaria Afrika	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
11	28 Aprili	Siku ya Veterinari Duniani	Wizara yenye dhamana ya Mifugo
12	04 Mei	Siku ya Walemavu wa ngozi (Maalbino)	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
13	07 Mei	Siku ya Mawasiliano	Wizara yenye dhamana ya Mawasiliano
14	15 Mei	Siku ya Familia Duniani	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto
15	18 Mei	Siku ya Makumbusho Duniani	Wizara yenye dhamana ya Utalii
16	26 Mei	Siku ya Wajane	Wizara yenye dhamana ya Jinsia na Watoto
17	30 Mei	Kuwasha Mwenge wa Uhuru	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
18	30 Mei	Siku ya Nishati na Madini	Wizara yenye dhamana ya Nishati
19	26 – 31 Mei	Wiki ya Umemejua (Solar Energy)	Wizara yenye dhamana ya Nishati
20	31 Mei	Siku ya kutotumia Tumbaku Duniani	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
21	1 Juni	Siku ya Kunywa Maziwa Duniani	Wizara yenye dhamana ya Mifugo
22	5 Juni	Siku ya Mazingira	Wizara yenye dhamana ya Mazingira
23	12 Juni	Siku ya Kupinga ajira kwa Mtoto	Wizara yenye dhamana ya Ajira
24	14 Juni	Siku ya Utoaji Damu kwa Hiari	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
25	16 Juni	Siku ya Mtoto wa Afrika	Wizara yenye dhamana ya Watoto
26	16-23 Juni	Wiki ya Utumishi wa Umma	Wizara yenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma
27	20 Juni	Siku ya Wakimbizi Duniani	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani/Wakimbizi

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
28	26 Juni	Siku ya kudhibiti Madawa ya Kulevya	Wizara yenye dhamana ya Kuratibu, Kudhibiti na Kuzuia Madawa ya Kulevya
29	1 Julai	Siku ya Serikali za Mitaa	Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
30	7 Julai	Siku ya Ushirika Duniani	Wizara yenye dhamana ya Ushirika
31	11 Julai	Siku ya Idadi ya Watu Duniani	Wizara yenye dhamana ya Idadi ya Watu
32	25 Julai	Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa	Wizara yenye dhamana ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa
33	1 Agosti	Siku ya Unyonyeshaji	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
34	12 Agosti	Siku ya Vijana Duniani	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana
35	25 Agosti	Siku ya Polisi Jamii	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
36	1 Septemba	Siku ya Majeshi	Wizara yenye dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
37	1-8 Septemba	Wiki ya Elimu ya Watu Wazima Duniani	Wizara yenye dhamana ya Elimu
38	8 Septemba	Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Mifugo
39	9-15 Septemba	Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani
40	15 Septemba	Siku ya Demokrasia Duniani	Wizara yenye dhamana ya Sheria
41	16 Septemba	Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni	Wizara yenye dhamana ya Mazingira
43	21 Septemba	Siku ya Michezo Tanzania	Wizara yenye dhamana ya Michezo
44	26 Septemba	Siku ya Unywaji Maziwa Mashuleni	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Mifugo
45	01 Oktoba	Siku ya Makazi Duniani	Wizara yenye dhamana ya Makazi

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
46	01 Oktoba	Siku ya Wanyama wa Mashambani	Wizara yenye dhamana Maendeleo ya Mifugo
47	01 Oktoba	Siku ya Usafirishaji	Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi
48	01 Oktoba	Siku ya Wazee Duniani	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii.
49	1-7 Oktoba	Wiki ya Wanyama Duniani	Wizara yenye Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
50	8 Oktoba	Siku ya Fimbo nyeupe	Wizara yenye dhamana ya Afya na Ustawi wa Jamii
51	10 Oktoba	Siku ya Maafa Duniani	Wizara yenye dhamana na Maafa
52	14 Oktoba	Kilele cha Wiki ya Vijana Tanzania	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana
53	15 Oktoba	Siku ya Wanawake Vijijini	Wizara yenye dhamana ya Jinsia kwa kushirikiana na Vyama visivyo vya Kiserikali
54	16 Oktoba	Siku ya Chakula Duniani	Wizara yenye dhamana ya Kilimo na Chakula

Na.	TAREHE	MAADHIMISHO/ SHEREHE	WIZARA/TAASISI HUSIKA
55	17 Oktoba	Siku ya kuondoa Umaskini Duniani	Wizara yenye dhamana ya Uchumi
56	24 Oktoba	Siku ya kupandisha Bendera ya Umoja wa Mataifa	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa
57	1 Novemba	Siku ya Sayansi na Elimu ya Juu	Wizara yenye dhamana ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu
58	5 Novemba	Siku ya Wavuvi Duniani	Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Uvuvi
59	1 Desemba	Siku ya UKIMWI Duniani	Wizara yenye dhamana ya masuala ya UKIMWI
60	10 Desemba	Siku ya Haki za Binadamu	Wizara yenye dhamana ya Sheria
61	10 Desemba	Siku ya Maadili	Taasisi ya Kupambana na kuzuia Rushwa

SEHEMU YA PILI

MUUNDO NA MAJUKUMU YA KAMATI

(a) KAMATI YA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Kutakuwa na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itakayosimamia na kuratibu Sherehe za Taifa. Mwenyekiti wa Kamati ni Waziri Mkuu na Katibu wake ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu. Kamati hii itajumuisha wafuatao:-

- | | | |
|--------|--|------------|
| (i) | Waziri Mkuu | Mwenyekiti |
| (ii) | Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Uratibu na Bunge) | Mjumbe |
| (iii) | Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora | Mjumbe |
| (iv) | Waziri mwenye dhamana ya Muungano | Mjumbe |
| (v) | Waziri mwenye dhamana na masuala
ya Fedha | Mjumbe |
| (vi) | Waziri mwenye dhamana na masuala
ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa
Kimataifa | Mjumbe |
| (vii) | Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI | Mjumbe |
| (viii) | Waziri mwenye dhamana na masuala
ya Elimu | Mjumbe |
| (ix) | Waziri mwenye dhamana na masuala
ya Ujenzi | Mjumbe |
| (x) | Waziri mwenye dhamana na masuala
ya Habari na Utamaduni | Mjumbe |
| (xi) | Waziri mwenye dhamana na masuala ya
Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | Mjumbe |

(xii)	Waziri mwenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi	Mjumbe
(xiii)	Mkuu wa Mkoa	Mjumbe
(xiv)	Katibu Mkuu Kiongozi	Mjumbe
(xv)	Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi	Mjumbe
(xvi)	Inspekta Jenerali wa Polisi	Mjumbe
(xvii)	Kamishna Mkuu wa Magereza	Mjumbe
(xviii)	Mkurugenzi Mkuu, Usalama wa Taifa	Mjumbe
(xix)	Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu	Katibu

MAJUKUMU YA KAMATI

Kamati itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia Maadhimisho na Sherehe kuu tatu za kitaifa ambazo ni:-

- (i) Sherehe za Uhuru na Jamhuri zinazofanyika tarehe 9 Desemba ya kila mwaka.
- (ii) Sherehe za Muungano zinazofanyika tarehe 26 Aprili ya kila mwaka.
- (iii) Maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa yanayofanyika tarehe 25 Julai ya kila mwaka.

Aidha, Kamati itashirikiana na Wizara nyingine kufanikisha maadhimisho mbalimbali ya Taifa. Maadhimisho hayo ni pamoja na:-

- (i) Sherehe za Mapinduzi Zanzibar zinazofanyika tarehe 12 Januari ya kila mwaka.
- (ii) Siku ya Kumbukumbu ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar inayoadhimishwa tarehe 7 Aprili ya kila mwaka.

- (iii) Sherehe za Siku ya Wafanyakazi zinazofanyika tarehe 1 Mei ya kila mwaka.
- (iv) Kilele cha Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayofanyika tarehe 7 Julai ya kila mwaka.
- (v) Sherehe za Siku ya Wakulima zinazofanyika tarehe 8 Agosti kila mwaka.
- (vi) Siku ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere inayoadhimishwa tarehe 14 Oktoba ya kila mwaka.

(b) KAMATI YAUTENDAJI YA MAADHIMISHO NA SHEREHE ZA TAIFA

Kamati hii itaundwa na wafuatao:-

- (i) Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mwenyekiti
- (ii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na TAMISEMI - Mjumbe
- (iii) Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu - Mjumbe
- (iv) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mjumbe
- (v) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na masuala ya Fedha - Mjumbe
- (vi) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mjumbe
- (vii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na masuala ya Elimu - Mjumbe
- (viii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na masuala ya Ujenzi - Mjumbe
- (ix) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na Masuala ya Habari na Utamaduni - Mjumbe
- (x) Katibu Tawala wa Mkoa mahali Sherehe itakapofanyika - Mjumbe

(xi) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi	- Mjumbe
(xii) Mkuu wa Jeshi la Polisi	- Mjumbe
(xiii) Mkurugenzi Mkuu, Usalama wa Taifa	- Mjumbe
(xiv) Kamishna Mkuu wa Jeshi la Magereza	- Mjumbe
(xv) Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa	- Mjumbe
(xvi) Mkurugenzi wa Jiji/ Manispaa/ Halmashauri	- Mjumbe
(xvii) Mkurugenzi, Maadhimisho na Sherehe za Taifa	- Katibu

Mwenyekiti wa Kamati anaweza kuwaalika wajumbe kutoka sehemu mbalimbali kama atakavyoona inafaa.

MGAWANYO WA MAJUKUMU

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu

- Mratibu Mkuu wa maandalizi ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.
- Kuandaa orodha ya waalikwa wa ndani ya nchi.
- Kuandaa kadi za mialiko.
- Kuandaa ratiba ya Sherehe.
- Kuandaa vifaa muhimu vinavyotumika wakati wa maadhimisho na Sherehe za taifa kama vipaza sauti, mazulia mekundu, mahema, vyoo vinavyohamishika, viti, na Luninga kubwa za nje.
- Kuandaa taratibu za usafiri wa viongozi mbalimbali watakaoshiriki katika Sherehe kwa kutumia mabasi.
- Kusimamia mapambo katika eneo la Sherehe kama vile maua, vipeperushi na mabango.
- Kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana katika eneo la Sherehe na maadhimisho kama vile maji, umeme na jenereta.

- Kuratibu ukarabati wa barabara zinazotumika wakati wa Sherehe.
- Kutunza kumbukumbu za matukio wakati wa Sherehe.
- Kuratibu na kuchambua makadirio ya Sherehe kutoka Wizara na Taasisi zinazohusika na maandalizi ya Sherehe na kuwasilisha Hazina kwa ajili ya kuombewa fedha.
- Kushirikiana na Mnikulu na Idara ya Itifaki kuandaa tafrija ya Sherehe za Taifa baada ya ratiba ya uwanjani.
- Kuandaa taratibu za malazi kwa waalikwa maalum kutoka ndani ya nchi.
- Kuhakikisha upatikanaji wa sare maalum kama fulana, kofia na vitenge katika Sherehe.
- Kuandaa majukwaa kwa ajili ya Viongozi Wakuu, Waandishi wa Habari na Wapiga picha pamoja na majukwaa kwa ajili ya burudani.

(ii) Ofisi ya Rais, Ikulu

- Kuandaa dhifa/tafrija kwa ajili ya sherehe za taifa kwa kushirikiana na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa na Idara ya Itifaki, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.
- Kusimamia mapokezi ya waalikwa wakati wa dhifa/tafrija.

(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais

- Kuwa kiungo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika masuala ya Sherehe za Kitaifa na

Maadhimisho mbalimbali.

- Kuratibu na kusimamia waalikwa kutoka Tanzania Bara/ Zanzibar /Tanzania Visiwani watakaohudhuria sherehe:-
 - Viongozi mbalimbali
 - Wageni maalum
 - Vijana wa uhamasishaji

(iv) Wizara yenye dhamana na Fedha

- Kuchambua makadirio ya Taasisi zinazoomba fedha za sherehe.
- Kuhakikisha fedha za Sherehe na Maadhimisho mbalimbali zinapatikana kwa wakati.

(v) Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

- Kuratibu masuala yote yanayohusiana na Taasisi za nje ya nchi zitakazoalikwa kuhudhuria katika Sherehe.
- Kuandaa na kusimamia mialiko ya Mabalazi wanaowakilisha nchi zao na wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa.
- Kuandaa na kusimamia mapokezi ya wageni kutoka nje ya nchi wanaohudhuria Sherehe za taifa.
- Kuandaa shada la maua kwa ajili ya Sherehe za Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa.
- Kusimamia masuala ya Itifaki katika Sherehe, mapokezi, kukaa na kutoka kwa Viongozi wa Taifa kwa kushirikiana na Kitengo cha Maadhimisho ya Sherehe za Taifa.
- Kuandaa taratibu za malazi ya waalikwa kutoka nje ya nchi.

- Kushirikiana na Ofisi ya Rais Ikulu na Kitengo cha Maadhimisho ya Sherehe za Taifa kuandaa tafrija/dhifa.
- Kuandaa tafrija/dhifa za Sherehe za Taifa.
- Kuratibu masuala ya usafiri wa Mabalazi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa wanapohudhuria Sherehe za kitaifa na maadhimisho mbalimbali.

(vi) Wizara yenye dhamana na Elimu/Wizara yenye dhamana na TAMISEMI

- Kuratibu na kusimamia maandalizi ya Kwaya ya Halaiki kwa kushirikiana na Mkoa husika.
- Kuandaa vijana wa michezo ya halaiki kutoka katika Shule za Msingi.
- Kuandaa vijana wa uhamasishaji kutoka katika Shule za Sekondari wakati wa sherehe kwa kushirikiana na Mkoa husika.
- Kusimamia upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya Vijana wa uhamasishaji.
- Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na sare maalum kwa ajili ya vijana wa michezo ya Halaiki.

(vii) Wizara yenye dhamana ya Habari na Utamaduni

- Kuratibu na kusimamia Waandishi wa Habari na Wapigapicha.
- Kusimamia utoaji wa vitambulisho maalum vya Sherehe na maadhimisho mbalimbali kwa Waandishi wa Habari na Wapigapicha.
- Kuandaa orodha ya Waandishi wa Habari na Wapiga picha kabla ya Sherehe na kuiwasilisha kwa Kamati ya Taifa.

- Kuandaa orodhaya Vyombo vya Habari vitakavyoshiriki katika Sherehe za taifa na kuwasilisha kwa Kamati ya Taifa.
- Kuhakikisha nidhamu kwa Waandishi wa Habari na Wapigapicha wakati wa kilele cha Sherehe za Kitaifa na Maadhimisho mbalimbali.
- Kushiriki katika kuandaa maeneo ya kukaa Waandishi wa Habari na Wapiga picha katika eneo la Sherehe.
- Kuhamasisha Waandishi wa Habari na Wapigapicha kushiriki katika mazoezi ya mwisho kabla ya Sherehe.
- Kutunza kumbukumbu za matukio yote yanayofanyika wakati wa Sherehe za kitaifa na kwenye maadhimisho mbalimbali.
- Kuandaa na kusimamia usafiri, mapokezi, malazi ya vikundi kutoka mikoani hadi eneo la Sherehe.
- Kuandaa orodha ya vikundi vya ngoma za asili kutoka mikoani na kuiwasilisha kwa Kamati ya Kitaifa.
- Kuhakikisha mavazi ya vikundi vya ngoma za asili yanaendana na uasili wa ngoma yenyewe.

(viii) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

- Kuratibu, kusimamia na kushiriki kwenye maandalizi ya gwaride la heshima.
- Kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo ya Sherehe kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.
- Kusimamia upatikanaji wa sare na vifaa vinavyotumika katika gwaride.

(ix) Jeshi la Polisi

- Kushiriki katika mazoezi na gwaride la heshima.
- Kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo yote ya Sherehe kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

- Kuhakikisha barabara zinazotumiwa na viongozi kwenda eneo la tukio zipo katika hali ya usalama.
- Kuongoza misafara ya magari ya viongozi mbalimbali kutoka maeneo tofauti hadi eneo la tukio.
- Kuhakikisha ulinzi na usalama kwenye milango wanapoinjilia waalikwa na wananchi, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.
- Kusimamia upatikanaji wa sare na vifaa vinavyotumika katika gwaride.

(x) Idara ya Usalama wa Taifa

- Kuweka mipango na utaratibu wa ulinzi na usalama katika maeneo yote ya matukio kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.
- Kuratibu na kuhakikisha usafiri wa viongozi wa kitaifa.
- Kuandaa vitambulisho kwa ajili ya wajumbe wa Kamati na watendaji mbalimbali.
- Kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo watakayofikia wageni waalikwa kutoka nje ya nchi watakaohudhuria Sherehe kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.
- Kukagua magari yatakayotumiwa na Viongozi mbalimbali kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

(xi) Jeshi la Magereza

- Kushiriki katika mazoezi na gwaride la heshima.
- Kushiriki katika Ulinzi na Usalama.
- Kusimamia upatikanaji wa vifaa vinavyotumika kwenye gwaride.

(xii) Halmashauri ya Jiji/Manispaa/Mji

- Kusimamia na kuratibu uwekaji wa bendera na mabango katika maeneo mbalimbali ya Jiji/Mji kwa kushirikiana na Mkoa.
- Kusimamia usafi wa Jiji/Mji kwa kushirikiana na Mkoa husika.

(c) KAMATI YA SHEREHE YA MKOA

Endapo Maadhimisho na Sherehe za Taifa zitafanyika nje ya Mkoa wa Dar es Salaam, Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaratibu na kusimamia maandalizi kwa kushirikiana na Kamati ya Sherehe ya Mkoa husika.

Kamati ya Sherehe ya Mkoa itahusisha wafuatao:-

- | | |
|--|--------------|
| (i) Mkuu wa Mkoa | - Mwenyekiti |
| (ii) Katibu Tawala wa Mkoa | - Katibu |
| (iii) Afisa Usalama wa Taifa wa Mkoa | - Mjumbe |
| (iv) Kamanda wa Polisi wa Mkoa | - Mjumbe |
| (v) Mkuu wa Magereza wa Mkoa | - Mjumbe |
| (vi) Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa | - Mjumbe |
| (vii) Afisa Uhamiaji wa Mkoa | - Mjumbe |
| (viii) Mshauri wa Mgambo wa Mkoa | - Mjumbe |
| (ix) “Base Commander” JWTZ/Kamanda Kikosi cha Jeshi. | - Mjumbe |
| (x) Wakuu wa Wilaya wote | - Mjumbe |
| (xi) Makatibu Tawala Wasaidizi Sekretarieti ya Mkoa | - Wajumbe |
| (xii) Wakurugenzi wa Halmashauri zote Mkoani | - Wajumbe |
| (xiii) Mkuu wa Hazina Ndogo | - Wajumbe |

Majukumu ya Kamati ya Sherehe ya Mkoa:-

- Kuhamasisha wananchi kushiriki katika Sherehe.
- Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Elimu kuandaa michezo ya Halaiki na wanafunzi wa uhamasishaji.
- Kuunda Kamati ndogondogo za utendaji kama vile:-
 - Kamati ya Burudani, Habari na Uhamasishaji
 - Kamati ya Chakula na Afya
 - Kamati ya Ujenzi, Uwanja na Mapambo
 - Kamati ya Mapokezi, Usafiri na Malazi
 - Kamati ya Ulinzi na Usalama
- Kuratibu na kusimamia mapokezi na malazi kwa waalikwa.
- Kuandaa na kusimamia vijana wa uhamasishaji.
- Kuandaa na kusimamia vikundi vya burudani vitakavyoshiriki katika Sherehe kabla ya ratiba rasmi kuanza.
- Kuandaa mabango na kuyaweka katika sehemu za mji kwa kushirikiana na Jiji, Miji na Halmashauri.
- Kutoa tamko rasmi (Press release) kwa ajili ya kuwatangazia wananchi Sherehe husika kwenye vyombo vya habari.
- Kuandaa Bajeti ya Sherehe na kuwasilisha kwenye Kamati ya Mkoa/Kamati ya Utendaji.
- Kutoa taarifa kwa Kamati ya Utendaji ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

SEHEMU YA TATU

VIFAA NA VITENDO MUHIMU KATIKA SHEREHE ZA KITAIFA

(a) VIFAA

- (i) Mahema ya ukubwa mbalimbali.
- (ii) Viti kwa ajili ya Viongozi na waalikwa wengine.
- (iii) Vipaza Sauti.
- (iv) Majukwaa ya kukaa viongozi na ya burudani.
- (v) Mazulia mekundu.
- (vi) Luninga kubwa za nje.
- (vii) Majukwaa kwa ajili ya Waandishi wa Habari na Wapigapicha.
- (viii) Majukwaa ya kuzungumzia.
- (ix) Jukwaa dogo kwa ajili ya mgeni rasmi kupokelea heshima.
- (x) Mabasi kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa na watendaji wakuu.
- (xi) Vitambulisho vya makundi mbalimbali.
- (xii) Silaha za asili kama vile Ngao, Mkuki, Sime, Upinde, Mishale na Shoka.
- (xiii) Bendera ya Taifa na mataifa mbalimbali (ndogo na kubwa), vipeperushi, mabango na milingoti ya Bendera.
- (xiv) Jenereta za Umeme zinazohamishika.
- (xv) Vyoo vinavyohamishika.
- (xvi) Mapambo na mashada ya maua.
- (xvii) Sare maalum kama vile Vitenge, kanga, nguo za michezo, fulana na kofia.

(b) VITENDO MUHIMU

Sherehe za Kitaifa zitafanikishwa kwa kuhusisha miongoni mwa mambo yafuatayo:-

- (i) Gwaride la heshima linaloandaliwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama (JWTZ, JKT, POLISI na MAGEREZA).
- (ii) Onesho la askari wa miavuli.
- (iii) Uoneshaji wa silaha mbalimbali za kivita kama vile mizinga, ndege za usafirishaji, ndege za kivita na vifaru.
- (iv) Michezo ya halaiki ya wanafunzi wa shule za msingi.
- (v) Vikundi maalum vya ngoma za asili kutoka sehemu mbalimbali nchini.
- (vi) Wimbo maalum unaoandaliwa na kikundi kitakachoteuliwa.
- (vii) Hotuba ya mgeni rasmi.
- (viii) Vikundi mbalimbali vya Burudani (maonesho ya brass band, matarumbeta, muziki wa dansi na sarakasi).
- (ix) Fashifashi/Fataki.
- (x) Ving'ora na honi za meli, gari moshi na magari.
- (xi) Maandamano ya wapanda pikipiki na baiskeli.
- (xii) Maonesho ya Farasi na Mbwa waliofundishwa.
- (xiii) Njiwa weupe kurushwa.
- (xiv) Kaulimbiu ya kila mwaka wakati wa sherehe, kupitishwa na kamati.
- (xv) Wananchi kushirikishwa katika kufanikisha sherehe.
- (xvi) Maandamano ya Wananchi
- (xvii) Tafrija.
- (xviii) Dua na Sala.
- (xix) Maonesho ya shughuli za Wizara/Idara mbalimbali.
- (xx) Michezo mbalimbali.
- (xxi) Kongamano na washa.

SEHEMU YA NNE

SHEREHE ZA UHURU NA JAMHURI

Sherehe za Uhuru na Jamhuri zitaadhimishwa tarehe 9 Desemba ya kila mwaka katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam sehemu ambapo Uhuru ulipatikana. Sherehe hizi zinaweza kuadhimishwa nje ya Mkoa wa Dar es Salaam kama itakavyoelekezwa na Kamati ya Taifa. Hatua za maandalizi ya sherehe hizi ni kama ifuatavyo:-

(a) Taarifa

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kuhusu Sherehe husika. Taarifa itatolewa angalau miezi mitatu kabla ya Sherehe.

(b) Vikao vya Kamati ya Maandalizi

Kutakuwa na vikao visivyozidi sita (6) vya maandalizi ya sherehe na kikao kimoja cha tathmini.

- (i) Kikao cha kwanza kitakuwa cha kupanga na kupeana maelekezo ya aina ya sherehe na mahali zitakapofanyika.
- (ii) Kikao cha pili ni cha kuwasilisha makadirio ya gharama za sherehe.
- (iii) Kikao cha tatu ni cha taarifa za utekelezaji wa majukumu.
- (iv) Kikao cha nne ni cha kupata taarifa ya mwisho ya maandalizi kwa kupitia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika kikao cha 1, 2 na 3.

- (v) Kikao cha tano ni cha mazoezi kwa vitendo katika eneo la tukio. Kikao hiki kitahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari na Wapigapicha.
- (vi) Kikao cha sita ni cha tathmini ya Maadhimisho ya Sherehe kikao hicho kifanyike ndani ya wiki mbili baada ya sherehe.

Endapo sherehe hizi zitafanyika nje ya Dar es Salaam kutakuwa na vikao visivyozidi vitano vya Kamati ya Taifa pamoja na Kamati ya Sherehe ya Mkoa. Aidha, Kamati ya Sherehe ya Mkoa itakuwa na vikao vitatu vya kutoa taarifa ya utekelezaji kama ilivyoorodheshwa hapo juu.

(c) Ratiba

- Ratiba itazingatia yafuatayo:-
 - Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
 - Muda
 - Matukio
 - Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba ikamilishwe mwezi mmoja kabla ya kilele cha Sherehe na kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kwa ajili ya kupitishwa.

(d) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa itaandaliwa miezi miwili kabla ya sherehe ili kuruhusu uandaaji wa barua na kadi za mialiko.

1. Barua za Mialiko

Barua za mialiko zitatayarishwa kwa ajili ya makundi yafuatayo:-

- (i) Viongozi kutoka nje ya nchi ambao wataalikwa kuhudhuria Sherehe.
- (ii) Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.
- (iii) Jaji Mkuu na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo madarakani na wastaafu.
- (iv) Spika wa Baraza la Wawakilishi na Jaji Mkuu Zanzibar waliopo madarakani na wastaafu.
- (v) Katibu Mkuu Kiongozi.
- (vi) Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.
- (vii) Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).
- (viii) Viongozi wa Dini ngazi ya Taifa (BAKWATA, CCT, TEC).
- (ix) Waalikwa wengine kama itakavyoelekezwa na Kamati.

Aidha, makundi yaliyotajwa hapo juu yatapelewa kadi za mialiko ya uwanjani isipokuwa Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

Kadi za mialiko ya tafrija na dhifa zitatolewa kwa makundi yote yaliyotajwa hapo juu isipokuwa Rais.

2. Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitatayarishwa kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Watakaopewa kadi za mialiko ni Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Makatibu Wakuu, Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Taasisi na Idara Zinazojitegemea, Wakurugenzi katika Wizara, Viongozi wa Dini ngazi ya Taifa na Wafanyabiashara mbalimbali.

(e) Gwaride

Kutakuwa na Gwaride la Heshima lenye gadi 10 zitakazohusisha vikosi vya Majeshi ya Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

(i) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

- Gadi 1 ya Wanaume (Jeshi la nchi kavu)
- Gadi 1 ya Wanawake (Jeshi la nchi kavu)
- Gadi 1 ya Wanaume (Jeshi la wanaanga)
- Gadi 1 ya Wanaume (Jeshi la wanamaji)

(ii) Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

(iii) Jeshi la Polisi

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

(iv) Jeshi la Magereza

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

Vikundi Ambatishi

- Kikundi cha Bendi (JWTZ)
- Kikundi cha Bendera (JWTZ)
- Kikundi cha Mizinga (JWTZ)
- Kikundi cha “Fanfare” (JWTZ)
- Kikundi cha Bendi (JKT)
- Kikundi cha Bendi (Polisi)
- Kikundi cha Bendi (Magereza)

Vitendo vya Gwaride

- Gwaride kuingia uwanjani.
- Kamanda wa gwaride kuchukua uongozi wa gwaride.
- Viongozi Wakuu wa kitaifa kuingia Uwanjani kwa mpangilio maalum.
- Rais na Amiri Jeshi Mkuu akifuatana na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kuwasili uwanjani wakiwa kwenye gari maalum na “fanfare” kupigwa.
- Gwaride litatoa salaam ya Rais ikiambatana na wimbo wa Taifa na mizinga 21 kupigwa wakati Rais akiwa kwenye jukwaa dogo la kupokelea heshima (saluting dais).
- Kamanda wa gwaride atamkaribisha Rais kukagua gwaride.
- Rais atakagua gwaride la heshima
- Rais atakwenda jukwaa kuu.
- Gwaride litapita mbele kwa heshima kwa mwendo wa pole na mwendo wa haraka.
- Gwaride litasonga mbele hatua kumi na tano kwa mwendo wa haraka.
- Gwaride litatoa salaam ya Rais na wimbo wa Taifa utapigwa.
- Gwaride litatoa heshima ya utii kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu.
- Gwaride litatoka nje ya uwanja na kutawanyika rasmi.
- “Brass Band” itaingiza vikundi vya halaiki.
- Rais ataondoka uwanjani wakati bendi ya Jeshi ikipiga “Regimental March”.

Muundo na Utaratibu huu wa gwaride unaweza kubadilika kutokana na mahitaji ya wakati

(f) Michezo ya Halaiki

- (i) Katika sherehe hizi kutakuwa na michezo ya Halaiki ya wanafunzi wa shule za msingi.
- (ii) Usimamizi wa maandalizi ya halaiki ni jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI/Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Mkoa Sherehe zinapofanyika.
- (iii) Washiriki wa Halaiki watatakiwa kuvaa sare maalum kama vile fulana, kofia, au vazi la michezo.
- (iv) Halaiki itafanya onesho baada ya gwaride kutoka uwanjani.
- (v) Mazoezi ya Halaiki yatafanywa sambamba na mazoezi ya gwaride.

(g) Ngoma za Asili

- (i) Kutakuwa na vikundi vya ngoma za asili kutoka sehemu mbalimbali nchini kulingana na maelekezo yatakayotolewa na kamati. Vikundi vitatu vitatoka Tanzania Bara na kimoja kitatoka Zanzibar. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati anaweza kuelekeza vinginevyo kuhusu vikundi vya kualikwa kadri atakavyoona inafaa.
- (ii) Vikundi hivyo vitaratibiwa na Wizara yenye dhamana na Utamaduni (Idara ya Utamaduni).
- (iii) Vikundi vitachaguliwa kwa kuzingatia ubora.
- (iv) Vikundi vitakavyoshiriki vitatakiwa kufika katika eneo la tukio juma moja (siku 7) kabla ya sherehe.
- (v) Vikundi vitakavyoteuliwa vitatoa burudani uwanjani na kwenye tafrija itakayoandaliwa baada ya sherehe za uwanjani.

- (vi) Wanavikundi wanatakiwa wakae mahali pamoja ili iwe rahisi kufanya mazoezi ya mwisho.
- (vii) Maudhui ya nyimbo za vikundi na ngoma za asili yazingatie kauli mbiu ya sherehe.
- (viii) Mavazi yatazingatia uasili wa ngoma.

(h) Hotuba ya Mgeni Rasmi

Katika Sherehe hizi kutakuwa na hotuba mbili katika kipindi cha miaka mitano.

- (i) Hotuba moja itatolewa katika Sherehe ya kwanza baada ya Serikali mpya kuingia madarakani.
- (ii) Hotuba nyingine itatolewa katika Sherehe ya mwisho kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika.

Aidha, hotuba nyingine zitatolewa kila baada ya Miaka 25 ya sherehe za Uhuru.

Rasimu ya Hotuba itaandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na ikamilike mwezi mmoja kabla ya sherehe. Rasimu ya hotuba hiyo itawasilishwa kwa mgeni Rasmi kwa hatua zake.

(i) Wimbo Maalum

Kutakuwa na wimbo maalum utakaoimbwa kwa kuzingatia kaulimbiu. Wimbo utaimbwa na kikundi ambacho kitateuliwa.

(j) Vikundi mbalimbali vya Sanaa

Vikundi visivyozidi vinne vya burudani vitaandaliwa na vitatumbuiza kabla ya mgeni rasmi kuingia uwanjani.

(k) Fashifashi/Fataki

- (i) Fashifashi zitarushwa katika Sherehe kama itakavyoonekana inafaa.
- (ii) Urushwaji wa fashifashi utafanyika katika maeneo yatakayochaguliwa na Kamati.
- (iii) Viongozi mbalimbali wataalikwa kushuhudia urushaji wa fashifashi.
- (iv) Urushaji fashifashi utaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

(1) Mapambo

Kutakuwa na mapambo uwanjani, barabarani na sehemu mbalimbali katika eneo linalohusika na Maadhimisho kama ifuatavyo:-

- (i) Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itahusika na upambaji wa uwanja au sehemu ambapo sherehe zitafanyika. Mapambo yatakuwa ya maua na Bendera kwa upande wa uwanjani. Bendera na mabango vitawekwa katika sehemu mbalimbali za Mji.
- (ii) Uwekaji wa Bendera na Mabango utasimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji/Mji.
- (iii) Usafi wa Miji/Jiji na barabara utasimamiwa na Uongozi wa Mkoa na Jiji.
- (iv) Bendera ndogo za Taifa na vipeperushi vitaandaliwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(m) Barabara

Barabara ambazo hutumika kwa ajili ya misafara ya Viongozi wa Kitaifa na wakati wa Sherehe za Kitaifa zinatakiwa kuwa katika hali nzuri wakati wote. Wizara

yenye dhamana ya barabara isimamie matengenezo na utunzaji wa barabara hizo.

(n) Wapanda Pikipiki na Baiskeli

Yataandaliwa maandamano ya wapanda pikipiki na baiskeli katika sherehe kama itaonekana inafaa. Uhamasishaji wa wapanda pikipiki na baiskeli utasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Jiji na Jeshi la Polisi.

(o) Farasi na Mbwa

Kutakuwa na maonesho ya Farasi na Mbwa waliofundishwa yatakayosimamiwa na Jeshi la Polisi. Maonesho hayo yatafanyika katika sherehe kama itaonekana inafaa.

(p) Njiwa weupe/Maputo

Kutakuwa na urushwaji wa njiwa weupe na maputo katika sherehe kama itaonekana inafaa. Urushwaji wa njiwa weupe na maputo utasimamiwa na uongozi wa Jiji/Mkoa sherehe zitakapofanyika.

(q) Vifaa vitakavyohitajika uwanjani ni pamoja na vifuatavyo:-

(i) Mahema

Kutakuwa na mahema ya ukubwa mbalimbali kwa ajili ya mahitaji mbalimbali. Uwekaji wa mahema utaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(ii) Viti

Vitaandaliwa viti kwa ajili ya viongozi wa Kitaifa kwenye meza kuu na waalikwa wengine uwanjani.

(iii) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya kufuatilia matukio.

(iv) Jukwaa la Viongozi

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa jukwaa la Viongozi wa Kitaifa mahali ambapo sherehe zitafanyikia.

(v) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa.

(vi) Luninga kubwa za nje

Zitakuwepo luninga kubwa ndani na nje ya Uwanja kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kufuatilia matukio vizuri.

(vii) Majukwaa

Kutakuwa na majukwaa kwa ajili ya Waandishi wa Habari na Wapigapicha ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Jukumu hili litaratibiwa na Wizara yenye dhamana na vyombo vya Habari.

(viii) Sare Maalum

Kutakuwa na sare maalum kwa ajili ya vijana wa uhamasishaji na wa michezo ya halaiki. Sare hizo ni fulana na kofia, kanga au vitenge na sare za michezo. Sare zitaandaliwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi

ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Sare zitakazoandaliwa zivaliwe siku ya sherehe.

(ix) Jukwaa dogo la heshima

Kutakuwa na jukwaa dogo la kupokelea heshima mgeni rasmi litakaloandaliwa na kusimamiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

(x) Mabasi

Kutakuwa na mabasi kwa ajili ya usafiri wa pamoja wa Viongozi wa Kitaifa na Watendaji Wakuu yatakayowasafirisha kutoka sehemu ya mkusanyiko itakayokubalika hadi Uwanja wa Uhuru au eneo la tukio na kuwarudisha mara baada ya sherehe kuisha. Magari hayo yatakaguliwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama kabla ya kutumika.

(xi) Vitambulisho

Kutakuwa na vitambulisho vya wajumbe wa Kamati ya Maadhimisho ya Taifa vyenye picha na majina vitakavyotumika katika kila sherehe. Vile vile, kutakuwa na vitambulisho vya muda vya watendaji wa makundi mbalimbali kwa ajili ya sherehe hizi. Vitambulisho vitaandaliwa na kuratibiwa na Idara ya Usalama wa Taifa.

(xii) Jenereta

Kutakuwa na Jenereta uwanjani kwa ajili ya dharura ya umeme. Jenereta liwepo uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe.

(xiii) Vifaa vya huduma ya kwanza

Kutakuwa na vifaa vya huduma ya kwanza uwanjani ikiwa ni pamoja na gari la wagonjwa.

(r) Waandishi wa Habari

Waandishi wa Habari wataingia katika sherehe kwa kutumia vitambulisho maalum vitakavyotolewa na Idara ya Usalama wa Taifa. Waandishi hao wanatakiwa kuvaa nadhifu. Aidha, watatakiwa kuhudhuria mazoezi ya mwisho ya sherehe hizo kwa tarehe itakayopangwa.

(s) Itifaki

(i) Mapokezi

Mapokezi ya Viongozi wa Kitaifa waliopo Madarakani, Wastaafu pamoja na Viongozi wa Kimataifa watakapoingia Uwanjani watapokelewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Maadhimisho ya Taifa na Mkuu wa Mkoa. Viongozi hao watakaopokea wageni watavaa suti nyeusi. Kwa Wanaume suti itavaliwa pamoja na shati jeupe na tai nyekundu.

(ii) Itifaki ya Viongozi kuingia katika uwanja wa Sherehe ni kama ifuatavyo:-

- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Naibu Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu wastaafu
- Jaji Mkuu Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar

- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Marais Wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Makamu wa Rais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Waziri Mkuu
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(iii) Utaratibu wa Viongozi kukaa katika jukwaa kuu.

Utaratibu wa Viongozi kukaa katika Jukwaa Kuu utazingatia itifaki. Kimsingi utakuwa kama ulivyooneshwa katika bango kitita (jedwali) hapa chini.

MFANO WA MPANGO WA UKAAJI WA VIONGOZI WA KITAIFA

1	RC										13	SPIKA WA BUNGE LA JAMHURITYA MUUNGANO
2	JAJI MKUU										12	RAIS MSTAAFU AWAMU YA TATU
3	RAIS MSTAAFU AWAMU YA PILI										11	MKE WA RAIS ZINZ
4	MI RAI S ZINZ										10	WAZIRI MKUU
5	MAKAMU WA RAI S										9	MKE WA RAIS
6	CDF										8	RAIS WA ZINZ
7											7	
8											6	
9											5	
10											4	
11											3	
12											2	
13											1	
14	MII RAIS ZINZ										26	MKE WA RAIS WA ZINZ MSTAAFU
15	MKE WA WAZIRI MKUU										25	MKE WA RAIS MSTAAFU WA ZINZ
16	RAIS MSTAAFU ZINZ										24	MKE WA MAKAMU WA RAI S
17	WAZIRI MKUU NA MAKAMU WA KWANZA WA RAI S MSTAAFU										23	SPIKA MSTAAFU WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO
18											22	MAMA MARTA
19											21	ADC ZINZ
20											20	ADC
21											19	ADC
22											18	MAMA FATMA KARUME
23											17	
24											16	
25											15	
26											14	
27											13	
28											12	
29											11	
30											10	
31											9	
32											8	
33											7	
34											6	
35											5	
36											4	
37											3	
38											2	
39											1	
40											62	RESERVE
41											61	RESERVE
42											60	RESERVE
43											59	RESERVE
44											58	RESERVE
45											57	RESERVE
46											56	RESERVE
47											55	RESERVE
48											54	RESERVE
49											53	RESERVE
50											52	RESERVE
51											51	RESERVE

(iv) Itifaki ya Viongozi kuondoka uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais wastaafu
- Marais wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu Zanzibar
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar

(t) Bendera

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Bendera ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

(u) Tafrija

- (i) Kutakuwa na tafrija au chakula cha usiku IKULU baada ya sherehe za uwanjani.
- (ii) Waalikwa watapewa kadi za mialiko zitakazoandaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

Waalikwa hao ni:-

- Viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani na waliostaafu.
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Jaji Mkuu wa Zanzibar.
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).
- Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa.
- Majaji.
- Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa.
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
- Makamanda Waandamizi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
- Viongozi wa Mkoa na Wabunge wa mahali ambapo sherehe zitaadhimishwa.
- Wakuu wa Taasisi na Idara Zinazojitegemea kama itakavyoelekezwa na Kamati.
- Wastaafu wa ngazi mbalimbali wataalikwa kama itakavyoelekezwa na Kamati.
- Wawakilishi wa Wazee wa Mkoa sherehe zinapofanyikia.

- Wafanyabiashara wataalikwa kama itakavyoelekezwa na Kamati.
 - Viongozi wa Dini ngazi ya Taifa (BAKWATA, CCT na TEC).
- (iii) Tafrija itaandaliwa na Ofisi ya Rais, Ikulu kwa kushirikiana na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.
- (iv) Tafrija hiyo itazingatia uwepo wa mahema, viti, vipaza sauti, majukwaa, mazulia mekundu, vikundi vya burudani na “brass band”.
- (v) Maandalizi ya huduma mbalimbali yatazingatia uwepo wa watendaji kama vile askari, madereva na wahudumu.

SEHEMU YA TANO

SHEREHE ZA MUUNGANO

Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zitafanyika tarehe 26 Aprili ya kila mwaka katika uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam mahali ambapo udongo wa Tanganyika na Zanzibar ulichanganywa. Sherehe hizo zinaweza kufanyika nje ya Dar es Salaam kama Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itakavyoelekeza. Hatua za maandalizi ya sherehe hizi ni kama ifuatavyo:-

(a) Taarifa

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kuhusu sherehe husika. Taarifa itatolewa miezi mitatu kabla ya sherehe.

(b) Vikao vya Kamati

Kutakuwa na vikao visivyozidi sita (6) vya maandalizi ya sherehe na kikao kimoja (1) cha tathmini.

- (i) Kikao cha kwanza kitakuwa cha kupeana maelezo ya aina ya sherehe na mahali zitakapofanyika.
- (ii) Kikao cha pili ni cha kuwasilisha makadirio ya gharama za sherehe.
- (iii) Kikao cha tatu ni cha taarifa za utekelezaji wa majukumu.
- (iv) Kikao cha nne ni cha kupata taarifa ya mwisho ya maandalizi kwa kupitia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika kikao cha kwanza, cha pili na cha tatu.

- (v) Kikao cha tano ni cha mazoezi kwa vitendo katika eneo la tukio. Kikao hiki kitahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari na Wapigapicha.
- (vi) Kikao cha sita ni cha tathmini ya Maadhimisho/ Sherehe. Kikao kifanyike ndani ya wiki mbili baada ya sherehe.

Endapo sherehe hizi zitafanyika nje ya Mkoa wa Dar es Salaam kutakuwa na vikao visivyozidi vitano vya Kamati ya Maadhimisho ya Taifa na Kamati Sherehe ya Mkoa. Aidha, kamati ya sherehe ya Mkoa itakuwa na vikao vitatu vya peke yake vya kuandaa taarifa za utekelezaji wa maelekezo na maagizo ya vikao vya hapo juu.

(c) Ratiba

- Ratiba itazingatia yafuatayo:-
 - Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
 - Muda
 - Matukio
 - Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba ikamilishwe mwezi mmoja kabla ya kilele cha sherehe na kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho ya Taifa kwa ajili ya kupitishwa.

(d) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa itaandaliwa miezi miwili kabla ya sherehe ili kuruhusu uandaaji wa kadi na barua za mialiko.

1. Barua za Mialiko

Barua za mialiko zitatayarishwa kwa ajili ya makundi yafuatayo:-

- (i) Viongozi kutoka nje ya nchi ambao wataalikwa kuhudhuria sherehe.
- (ii) Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.
- (iii) Jaji Mkuu na Spika wa Bunge waliopo madarakani na wastaafu.
- (iv) Spika wa Baraza la Wawakilishi na Jaji Mkuu Zanzibar.
- (v) Viongozi wa Vyama vya Siasa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).
- (vi) Viongozi wa Dini ngazi ya Taifa (BAKWATA, CCT na TEC).
- (vii) Katibu Mkuu Kiongozi.
- (viii) Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi Zanzibar.
- (ix) Waalikwa wengine kama itakavyoelekezwa na Kamati.

Aidha, makundi yaliyotajwa hapo juu yatapewa kadi za mialiko isipokuwa Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

2. Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitatayarishwa kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Watakaopewa kadi za mialiko ni pamoja na Mawaziri, Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea, Wakurugenzi katika Wizara za Serikali, Viongozi wa Dini na Wafanyabiashara.

(e) Gwaride

Kutakuwa na Gwaride la Heshima lenye gadi 10 zitakazohusisha vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama kama ifuatavyo:-

(i) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

- Gadi 1 ya Wanaume (Jeshi la nchi kavu)
- Gadi 1 ya Wanawake (Jeshi la nchi kavu)
- Gadi 1 ya Wanaume (Jeshi la wanaanga)
- Gadi 1 ya wanaume (Jeshi la wanamaji)

(ii) Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

(iii) Jeshi la Polisi

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

(iv) Jeshi la Magereza

- Gadi 1 ya Wanaume
- Gadi 1 ya Wanawake

Vikundi Ambatishi

- Kikundi cha Bendi (JWTZ)
- Kikundi cha Bendera (JWTZ)
- Kikundi cha Mizinga (JWTZ)
- Kikundi cha “Fanfare” (JWTZ)
- Kikundi cha Bendi (JKT)
- Kikundi cha Bendi (Polisi)
- Kikundi cha Bendi (Magereza)

Vitendo vya Gwaride

- Gwaride kuingia uwanjani
- Kamanda wa gwaride kupokea gwaride
- Viongozi wakuu wa kitaifa kuingia uwanjani kwa mpangilio maalum.
- Rais na Amiri Jeshi Mkuu akifuatana na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kuingia uwanjani wakiwa kwenye gari maalum na “fanfare” kupigwa.
- Gwaride litatoa salaam ya Rais na wimbo wa Taifa utapigwa sambamba na mizinga 21 kupigwa wakati Rais akiwa kwenye jukwaa dogo la kupokelea heshima.
- Kamanda wa gwaride atamkaribisha Rais kukagua gwaride.
- Rais atakagua gwaride la heshima
- Rais atakwenda jukwaa kuu.
- Gwaride litapita mbele kwa heshima kwa mwendo wa pole na mwendo wa haraka.
- Gwaride litasonga mbele kwa heshima.
- Gwaride litatoa salaam ya Rais na wimbo wa Taifa utapigwa.
- Gwaride litatoa heshima ya utii kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu.
- Gwaride litatoka nje ya uwanja na kutawanyika rasmi.
- “Brass Band” itaingiza vikundi vya halaiki.
- Rais ataondoka uwanjani wakati bendi ya Jeshi ikipiga “Regimental March”.

Muundo na utaratibu wa gwaride unaweza kubadilika kutokana na mahitaji ya wakati.

(f) Michezo ya Halaiki

- (i) Katika sherehe hizi kutakuwa na michezo ya Halaiki ya wanafunzi wa shule za msingi.
- (ii) Usimamizi wa maandalizi ya michezo ya halaiki ni jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu /TAMISEMI Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Mkoa sherehe zitakapofanyika.
- (iii) Washiriki wa michezo ya halaiki watatakiwa kuvaa sare kama vile fulana, kofia, au vazi la michezo.
- (iv) Halaiki itafanya onesho baada ya gwaride kutoka uwanjani.
- (vi) Mazoezi ya michezo ya halaiki yatafanywa sambamba na mazoezi ya gwaride.

(g) Ngoma za Asili

- (i) Kutakuwa na vikundi vya ngoma za asili kutoka sehemu mbalimbali nchini kulingana na maelekezo yatakayotolewa na Kamati. Vikundi vitatu vitatoka bara na kimoja kitatoka Zanzibar. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati anaweza kuelekeza vinginevyo kuhusu vikundi vya kualika kadri atakavyoona inafaa.
- (ii) Vikundi hivyo vitaratibiwa na Wizara yenye dhamana na Utamaduni (Idara ya Utamaduni).
- (iii) Vikundi vitachaguliwa kwa kuzingatia ubora.
- (iv) Vikundi vitakavyoteuliwa vitatakiwa kufika katika eneo la tukio juma moja (siku 7) kabla ya sherehe.
- (v) Vikundi vitakavyoteuliwa vitatoa burudani uwanjani na kwenye tafrija itakayoandaliwa baada ya sherehe za uwanjani.
- (vi) Wanavikundi wanatakiwa wakae pamoja ili iwe rahisi kufanya mazoezi ya mwisho.
- (vii) Maudhui ya nyimbo na ngoma za asili za vikundi

yatazingatia kauli mbiu ya sherehe.

(viii) Mavazi yazingatie uasili wa ngoma.

(h) Hotuba ya Mgeni Rasmi

Katika sherehe hizi kutakuwa na angalau hotuba mbili katika kipindi cha miaka mitano.

(i) Hotuba moja itatolewa katika Sherehe ya kwanza baada ya Serikali mpya kuingia madarakani.

(ii) Hotuba nyingine itatolewa katika Sherehe ya mwisho kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika.

Aidha, hotuba nyingine zitatolewa kila baada ya miaka 25 ya Muungano. Rasimu ya Hotuba itaandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na ikamilike mwezi mmoja kabla ya sherehe. Rasimu ya hotuba hiyo itawasilishwa kwa mgeni rasmi kwa hatua zake.

(i) Wimbo Maalum

Kutakuwa na wimbo maalum utakaoimbwa kwa kuzingatia kaulimbiu. Wimbo utaimbwa na kikundi ambacho kitateuliwa.

(j) Vikundi Mbalimbali vya Sanaa

Vikundi visivyozidi vinne vya burudani vitaandaliwa na vitatumbuiza kabla ya mgeni rasmi kuingia uwanjani.

(k) Fashifashi/Fataki

(i) Fashifashi zitarushwa katika sherehe kama itakavyooneka inafaa.

(ii) Urushwaji wa fashifashi utafanyika katika eneo moja litakalochaguliwa na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(iii) Viongozi mbalimbali wataalikwa kushuhudia urushaji wa fashifashi.

- (iv) Urushwaji wa fashifashi utaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

(l) Mapambo

Kutakuwa na mapambo uwanjani, barabarani na sehemu mbalimbali za Mji/Jiji katika eneo linalohusika na maadhimisho.

- (i) Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itasimamia upambaji wa uwanja au sehemu ambapo sherehe zitafanyikia. Mapambo yatakuwa ya maua na Bendera kwa upande wa uwanjani. Bendera na mabango vitawekwa katika sehemu mbalimbali za Mji/Jiji.
- (ii) Uwekaji wa Bendera na Mabango utasimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji.
- (iii) Usafi wa Mji/Jiji na barabara utasimamiwa na Uongozi wa Mkoa na Jiji.
- (iv) Bendera ndogo za Taifa na vipeperushi vitaandaliwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(m) Barabara

Barabara zinazotumika kwa ajili ya misafara ya Viongozi wa Kitaifa na wakati wa Sherehe za Kitaifa zitawekwa katika hali nzuri wakati wote. Wizara yenye dhamana ya barabara itasimamia matengenezo na utunzaji wa barabara hizo.

(n) Wapanda Pikipiki na Baiskeli

Yataandaliwa maandamano ya wapanda pikipiki na baiskeli katika sherehe kama itakavyoonekana inafaa. Uhamasishaji wa wapanda pikipiki na baiskeli utasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Jiji na Jeshi la Polisi.

(o) Farasi na Mbwa

Kutakuwa na maonesho ya Farasi na Mbwa waliofundishwa yatakayosimamiwa na Jeshi la Polisi. Maonesho hayo yatafanyika katika sherehe kama itakavyoonekana inafaa.

(p) Njiwa weupe na Maputo

Kutakuwa na urushwaji wa njiwa weupe na maputo katika sherehe kama itakavyoonekana inafaa. Urushwaji wa njiwa na maputo utasimamiwa na kuratibiwa na uongozi wa Mji/Jiji sherehe zitakapofanyika.

(q) Vifaa

Vifaa vitakavyohitajika uwanjani ni pamoja na vifuatavyo:-

(i) Mahema

Kutakuwa na mahema ya ukubwa mbalimbali kwa ajili ya mahitaji mbalimbali. Uwekaji wa mahema utaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(ii) Viti

Vitaandaliwa viti kwa ajili ya viongozi wa Kitaifa kwenye meza kuu na waalikwa wengine uwanjani.

(iii) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya waalikwa na wananchi kufuatilia matukio.

(iv) Jukwaa la Viongozi

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa jukwaa la Viongozi wa Kitaifa, mahali ambapo sherehe zitafanyika.

(v) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa.

(vi) Luninga Kubwa za nje

Kutakuwepo luninga kubwa ndani na nje ya Uwanja kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kufuatilia matukio yanayoendelea vizuri.

(vii) Majukwaa

Kutakuwa na majukwaa kwa ajili ya waandishi wa habari na wapiga picha ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Majukwaa hayo yataratibiwa na Wizara yenye dhamana na vyombo vya Habari.

(viii) Sare Maalum

Kutakuwa na sare maalum kwa ajili ya vijana wa uhamasishaji wa michezo ya halaiki. Sare hizo ni fulana na kofia, kanga au vitenge na sare za michezo. Sare zitaandaliwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara ya Elimu. Sare zitakazoandaliwa zivaliwe siku ya sherehe.

(ix) Jukwaa dogo la heshima

Kutakuwa na jukwaa dogo kwa ajili ya kupokelea heshima mgeni rasmi litakaloandaliwa na kusimamiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

(x) Mabasi

Kutakuwa na mabasi kwa ajili ya usafiri wa pamoja wa Viongozi wa Taifa na Watendaji Wakuu yatakayowasafirisha kutoka sehemu ya mkusanyiko itakayokubalika hadi Uwanja wa Uhuru au eneo la tukio na kuwarudisha mara baada ya sherehe kuisha. Magari hayo yatakaguliwa na Vyombo Vya Ulinzi na Usalama kabla ya kutumika.

(xi) Vitambulisho

Kutakuwa na vitambulisho vya wajumbe wa kamati ya Maadhimisho ya Taifa vyenye picha na majina vitakavyotumika katika kila sherehe. Vile vile, kutakuwa na vitambulisho vya muda kwa ajili ya watendaji wa makundi mbalimbali kwa sherehe husika. Vitambulisho vitaandaliwa na kuratibiwa na Idara ya Usalama wa Taifa.

(xii) Jenereta

Kutakuwa na Jenereta uwanjani kwa ajili ya dharura ya umeme. Jenereta liwepo uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe.

(xiii) Vifaa vya huduma ya kwanza

Kutokana na vifaa vya huduma ya kwanza ikiwa ni pamoja na magari ya wagonjwa.

(xiv) Waandishi wa Habari

Waandishi wa Habari wataingia katika sherehe kwa kutumia vitambulisho maalum vitakavyotolewa na Idara ya Usalama wa Taifa. Waandishi hao watatakiwa kuvaa nadhifu.

Aidha, watatakiwa kuhudhuria mazoezi ya mwisho ya sherehe hizo kwa tarehe itakayopangwa.

(r) Tafrija

- (i) Kutakuwa na tafrija au dhifa itakayoandaliwa IKULU baada ya sherehe za uwanjani.
- (ii) Waalikwa watapewa kadi za mialiko zitakazoandaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

Waalikwa hao ni:-

- Viongozi wa Taifa waliopo madarakani na waliostaafu.
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Jaji Mkuu wa Zanzibar.
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).
- Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa.
- Majaji.

- Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa.
 - Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
 - Makamanda Waandamizi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.
 - Viongozi wa Mkoa na Wabunge wa Mkoa ambapo sherehe zitakapofanyikia.
 - Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea kama itakavyoelekezwa na Kamati.
 - Wastaafu wa ngazi mbalimbali wataalikwa kama itakavyoelekezwa na Kamati.
 - Wawakilishi wa Wazee wa Mkoa ambapo sherehe zitakapofanyika.
 - Wafanyabiashara wataalikwa kama itakavyoelekezwa na Kamati.
 - Viongozi wakuu wa Dini (BAKWATA, CCT na TEC).
- (iii) Tafrija au dhifa itaandaliwa na Ofisi ya Rais Ikulu kwa kushirikiana na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.
- (iv) Maandalizi ya tafrija hiyo yatazingatia uwepo wa mahema, viti, vipaza sauti, majukwaa, mazulia mekundu, vikundi vya burudani na “brass band”.
- (v) Maandalizi ya tafrija hiyo yatazingatia uwepo wa watendaji mbalimbali kama vile askari, madereva na wahudumu.

(s) Itifaki

- (i) Itifaki ya Viongozi kuingia katika uwanja wa sherehe ni kama ifuatavyo:-**
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
 - Katibu Mkuu Kiongozi

- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Spika Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Marais Wastaafu Zanzibar
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Waziri Mkuu
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Utaratibu wa Viongozi kukaa katika jukwaa kuu

Utaratibu wa Viongozi kukaa katika jukwaa kuu utazingatia itifaki na kimsingi utakuwa kama ulivyoonyeshwa katika bangokitita (jedwali) hapa chini.

MFANO WA MPANGO WA UKAAJI WA VIONGOZI WA KITAIFA

1 RC	2 JAJI MKUU	3 RAIS MSTAAFU AWAMU YA PILI	4 MAKAMU WA KIWANZA WA RAIS	5 MAKAMU WA RAIS	6 CDF	7	8 RAIS WA ZNZ	9 MKE WA RAIS	10 WAZIRI MKUU	11 MKE WA RAIS ZNZ	12 RAIS MSTA- AFU AWAMU YA TATU	13 SPIKA WA BUNGE LA JAMHURI YA MILUNG- ANO
51 MAKAMU WA PILI WA RAIS	52 RESERVE	53 RESERVE	54 RESERVE	55 RESERVE	56 RESERVE		57 RESERVE	58 RESERVE	59 RESERVE	60 RESERVE	61 RESERVE	62 RESERVE

(iii) Itifaki ya Viongozi kuondoka katika uwanja wa sherehe ni kama ifuatavyo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais wastaafu
- Marais wastaafu Zanzibar
- Makamu wa Rais wastaafu
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Zanzibar
- Mawaziri Wakuu wastaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi Zanzibar

(t) Bendera

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Bendera ya Jeshi la Ulinzi la wananchi wa Tanzania.

SEHEMU YA SITA

KUMBUKUMBU YA MASHUJAA

Maadhimisho ya kumbukumbu ya Mashujaa yatafanyika Kitaifa tarehe 25 Julai ya kila mwaka katika mojawapo ya sehemu yenye Mnara wa Uhuru na/au Makaburi ya Mashujaa popote nchini kama itakavyoelekezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

Maandalizi ya Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mashujaa yatajumuisha mambo yafuatayo:-

(a) Taarifa

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wa Kamati ya Maadhimisho kuhusu sherehe husika. Taarifa itatolewa miezi mitatu kabla ya siku ya Kumbukumbu.

(b) Vikao vya Maandalizi

Kutakuwa na vikao visivyozidi vitano (5) vya maandalizi vya Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

- (i) Kikao cha kwanza kitakuwa cha kupanga na kupeana maelezo ya mahali Maadhimisho yatakapofanyika.
- (ii) Kikao cha pili ni cha kuwasilisha na kujadili makadirio ya gharama za Maadhimisho.
- (iii) Kikao cha tatu ni cha taarifa za utekelezaji wa majukumu na utekelezaji wa yaliyokubalika katika kikao cha 1 na 2.

- (iv) Kikao cha nne ni kuona mazoezi kwa vitendo katika eneo la tukio. Kikao hicho kitahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari na Wapiga picha.
- (v) Kikao cha tano (5) ni cha tathmini baada ya Maadhimisho kufanyika. Kikao hicho kifanyike ndani ya siku (2) mbili baada ya Maadhimisho.

Endapo Maadhimisho hayo yatafanyika nje ya Dar es Salaam, kutakuwa na vikao vinne vya Maandalizi vya Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa na Kamati ya Sherehe ya Mkoa. Mkoa utakuwa na vikao vitatu vya maandalizi.

(c) Ratiba

Ratiba izingatie yafuatayo:-

- Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
- Muda
- Matukio
- Wahusika

Rasimu ya ratiba ikamilike mwezi mmoja kabla ya kilele cha maadhimisho na kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho kwa ajili ya hatua zaidi.

(d) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa itaandaliwa miezi miwili kabla ili kuwezesha uandaaji wa barua na kadi za mialiko kama ifuatavyo:-

(i) Barua za Mialiko

Barua za mialiko zitatayarishwa kwa ajili ya wafuatao:-

- Viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.
- Jaji Mkuu na Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo madarakani na wastaafu.
- Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Zanzibar.
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).
- Katibu Mkuu Kiongozi.
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.
- Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa ya jirani.
- Viongozi wa dini (BAKWATA, CCT na TEC)

(ii) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitatayarishwa kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Watakaopewa kadi za mialiko ni wafuatao:-

- Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makatibu Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Mabalози na wawakilishi wa mashirika ya Kimataifa
- Wazee waliopigana Vita dhidi ya Utawala wa Wakoloi nchini

- Askari waliopigana Vita kuu ya Kwanza na ya pili ya dunia (Tanzania Legion)
- Wawakilishi wa Wanajeshi waliopigana vita vya Kagera
- Wawakilishi wa Wanajeshi waliopigana katika vita mbalimbali za Ukombozi
- Wawakilishi wa Wazee wa Mkoa kama itakavyoelezwa na Mkoa
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama
- Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea
- Wakurugenzi wa Wizara

(e) **Gwaride**

Litaandaliwa Gwaride la Maombolezo lenye gadi nne (4) zinazohusisha Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

- Gadi moja ya wanaume

Vikundi Ambatishi

- Kikundi cha Mizinga
- Kikundi cha Maombolezo
- Kikundi cha Wapambe (ADCs)
- Kikundi cha “Military Band”
- Kikundi cha Wabeba silaha za jadi
- Kikundi cha Bendera
- Kikundi cha Buruji

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

- Gadi moja ya wanaume

Jeshi la Polisi

- Gadi moja ya wanaume

Jeshi la Magereza

- Gadi moja ya wanaume

(f) Mahitaji

Kutakuwa na mahitaji yafuatayo katika maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mashujaa:-

(i) Mapambo

Kutakuwa na mapambo ya Bendera sehemu ambayo maadhimisho hayo yatafanyikia.

(ii) Mahema

Kutakuwa na mahema kwa ajili ya wageni waalikwa na huduma mbalimbali. Uwekaji wa mahema utaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(iii) Viti

Kutakuwa na viti kwa ajili ya Viongozi wa Kitaifa na wageni waalikwa katika eneo la maadhimisho watakapokuwa wanasubiri ratiba rasmi kuanza.

(iv) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti katika maeneo ya matukio ambavyo vitaratibiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(v) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaandaa mazulia mekundu kwa ajili ya eneo watakapopita na kusimama Viongozi.

(vi) Silaha za Asili

Kutakuwa na Silaha za Asili zifuatazo:-
Ngao, Mkuki, Sime, Shoka, Upinde na Mishale. Silaha hizi zitasimamiwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(vii) Shada la Maua

Kutakuwa na Shada la Maua litakaloandaliwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

(viii) Majukwaa

Kutakuwa na majukwaa kwa ajili ya waalikwa mbalimbali. Majukwaa hayo yatakuwa na ngazi ili kuwawezesha waalikwa kuona vizuri.

(ix) Majukwaa

Kutakuwa na majukwaa kwa ajili ya Waandishi wa Habari na Wapigapicha ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Majukwaa haya yataandaliwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(x) Vazi Rasmi

Siku ya kumbukumbu ya Mashujaa waalikwa watavaa mavazi ya rangi nyeusi kama ishara ya

maombolezo. Waandishi wa Habari na Wapigapicha watavaa mavazi ya rangi nyeusi au utepe mweusi katika mkono wa kushoto.

(xi) Vitambulisho

Kutakuwa na vitambulisho vya wajumbe wa kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa vyenye picha na majina vitakavyotumika katika maadhimisho hayo. Vile vile kutakuwa na vitambulisho maalum vya muda kwa ajili ya makundi mbalimbali ya watendaji. Waandishi wa Habari wataingia katika eneo la tukio kwa vitambulisho maalum vitakavyotolewa na Idara ya Habari (MAELEZO). Vitambulisho vitaandaliwa na kuratibiwa na Idara ya Usalama wa Taifa.

(xii) Jenereta

Kutakuwa na Jenereta katika eneo la Maadhimisho kwa ajili ya dharura ya umeme. Jenereta liwepo katika eneo la tukio juma moja (1) kabla ya Maadhimisho.

(g) Maombolezo

Viongozi na waalikwa watasimama muda wote wa maombolezo kulingana na mtiririko wa vitendo vya maadhimisho ya kumbukumbu.

(h) Vitendo vya Maombolezo:

- Gwaride kujipanga nje ya uwanja.
- Kamanda kupokea gwaride.
- Kamanda wa gwaride kuingiza kikundi cha Bendera.

- Gwaride kuingia uwanjani.
- Viongozi mbalimbali wa Kitaifa kuwasili.
- Mkuu wa Majeshi kuwasili na kumpokea Rais.
- Rais akiongozana na Mkuu wa Majeshi kuingia eneo la maombolezo.
- Gwaride kutoa Salam ya Rais pamoja na Wimbo wa Taifa kupigwa.
- Kikundi cha Buruji kupiga “Last Post”
- Gwaride kuweka silaha begani.
- NCO na askari sita (6) kupindua silaha zao chini.
- Mizinga miwili kupigwa na watu wote kukaa kimya dakika moja.
- Gwaride kutoa “Present Arms”na Maafisa wenye Sare watapiga saluti.
- Kikundi cha Buruji kupiga Wimbo wa “Reveilles”.
- Gwaride kuteremsha Silaha na kufungua miguu.
- Kuweka silaha za Asili za Mashujaa na Shada la Maua kwenye Mnara wa Kumbukumbu ya Mashujaa;
 - (i) Rais ataweka Mkuki na Ngao
 - (ii) Mkuu wa Majeshi ataweka Sime
 - (iii) Kiongozi wa Mabalazi ataweka Shada la Maua
 - (iv) Mstahiki Meya wa Jiji/Mwenyekiti wa Halmashauri ataweka Upinde na Mishale
 - (v) Mwenyekiti wa “Tanzania Legion” ataweka Shoka
- Viongozi wa dini wafuatao watasoma dua na sala (BAKWATA, CCT na TEC)
- Gwaride kutoa heshima na Wimbo wa Taifa kupigwa
- Maafisa wenye sare watapiga saluti
- Mgeni Rasmi kuondoka

(i) Itifaki

(i) Itifaki ya Viongozi kuingia katika eneo la Kumbukumbu ya Mashujaa ni kama ifuatavyo:-

- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Jaji Mkuu Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Marais wastaafu Zanzibar
- Makamu wa Rais wastaafu
- Marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Waziri Mkuu
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(ii) Itifaki ya kuondoka katika eneo la Kumbukumbu ya Mashujaa ni kama ifuatavyo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais wastaafu Zanzibar
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu Zanzibar
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Naibu Waziri Kiongozi Mstaafu
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar

(iii) Bendera

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la Kumbukumbu ya Mashujaa ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Bendera ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

(j) Tafrija

Kutakuwa na tafrija au chakula cha mchana mara baada ya kumaliza ratiba ya shughuli za Kumbukumbu ya Mashujaa.

- Waalikwa watapewa kadi zitakazoandaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.
- Endapo maadhimisho haya yatafanyika Dar es Salaam wafuatao wataalikwa:-
 - (i) Wazee waliopigana vita dhidi ya utawala wa wakoloni nchini.
 - (ii) Askari waliopigana vita kuu ya kwanza na ya pili ya Dunia (Tanzania Legion).
 - (iii) Wawakilishi wa Wanajeshi waliopigana vita mbalimbali vya Ukombozi.
 - (iv) Viongozi wa Dini ngazi ya Taifa (BAKWATA, CCT na TEC).
 - (v) Mgeni rasmi atakayependekezwa na Kamati.
 - (vi) Viongozi wa Mkoa.
 - (vii) Wawakilishi wa askari walioshiriki gwaride.

Iwapo Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mashujaa yatafanyika nje ya Dar es Salaam viongozi wa Kitaifa wataalikwa.

SEHEMU YA SABA

SHEREHE ZA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar zitaadhimishwa Zanzibar tarehe 12 Januari ya kila mwaka. Mratibu na Msimamizi Mkuu wa sherehe hizi ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

(a) Itifaki

(i) Mapokezi

Mapokezi ya Viongozi wa Kitaifa waliopo Madarakani, Wastaafu pamoja na Viongozi wa Kimataifa watakapoingia Uwanjani watapokelewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mkuu wa Mkoa sherehe zitakapofanyika. Viongozi hao watakaopokea wageni watavaa suti nyeusi. Kwa Wanaume suti itavaliwa pamoja na shati jeupe na tai nyekundu.

(ii) Itifaki ya Viongozi wa Kitaifa kuingia uwanjani itakuwa kama ifuatavyo:-

- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Naibu Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Jaji Mkuu Zanzibar
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Mawaziri Wakuu Wastaafu
- Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Marais Wastaafu Zanzibar
- Makamu wa Rais Wastaafu
- Marais Wastaafu
- Waziri Mkuu
- Makamu wa Rais
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Rais wa Zanzibar

(iii) Itifaki ya Viongozi kuondoka

uwanjani ni kama ifuatavyo:-

- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais
- Waziri Mkuu
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar
- Marais wastaafu Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiduzi
- Marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Mawaziri Kiongozi Wastaafu
- Mawaziri Wakuu wastaafu
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Viongozi wa kitaifa wastaafu
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar

- Jaji Mkuu Zanzibar
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar

(b) **Gwaride**

Gwaride la sherehe hizi litaundwa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Polisi.

(c) **Bendera**

Bendera zitakazopepea siku ya sherehe ya Mapinduzi Zanzibar ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Bendera ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Bendera ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Zanzibar.

SEHEMU YA NANE

SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI (MEI MOSI)

Siku ya Wafanyakazi Duniani itaadhimishwa tarehe 1 Mei ya kila mwaka. Sherehe zitaratibiwa na kusimamiwa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya kazi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na Idara ya Maadhimisho ya Kitaifa. Sherehe hizi ni za kitaifa hivyo zitafuata itifaki zote zinazohusiana na sherehe za kitaifa. Wizara yenye dhamana na masuala ya kazi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania pamoja na wadau wengine itaandaa sherehe hizi.

(a) KAMATI YA MAANDALIZI

Kutakuwa na Kamati ya Maandalizi ya Sherehe ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yenye wajumbe wafuatao:-

- (i) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana- Mwenyekiti
- (ii) Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mjumbe
- (iii) Katibu Mkuu, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) - Mjumbe
- (iv) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Sekta ya Afya (TUGHE) - Mjumbe
- (v) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi wa Reli (TRAWU) - Mjumbe
- (vi) Katibu Mkuu, Chama cha

- Wafanyakazi katika mashamba
na Kilimo (TPWU) - Mjumbe
- (vii) Katibu Mkuu, Chama cha
Wafanyakazi wanaoshughulika na
Ulinzi (TUPSE) - Mjumbe
- (viii) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi
Sekta ya Mawasiliano (COTWU) - Mjumbe
- (ix) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi
wa Mahotelini na Majumbani
(CHODAWU) - Mjumbe
- (x) Katibu Mkuu, Chama cha
Wafanyakazi katika Serikali za
Mitaa (TALGWU) - Mjumbe
- (xi) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi
katika Migodi, Nishati na Ujenzi
(TAMICO) - Mjumbe
- (xii) Katibu Mkuu, Chama cha
Wafanyakazi wa Sekta ya Mawasiliano
ya Simu Tanzania (TEWUTA) - Mjumbe
- (xiii) Katibu Mkuu, Chama cha Wafanyakazi
katika Bandari (DOWUTA) - Mjumbe
- (xiv) Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe
za Taifa - Mjumbe
- (xv) Mwakilishi kutoka Idara ya Usalama
wa Taifa - Mjumbe
- (xvi) Mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa
Polisi - Mjumbe
- (xvii) Mkuu wa Itifaki, Wizara ya Mambo ya
Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mjumbe
- (xviii) Katibu Tawala wa Mkoa,
zitakapofanyika sherehe - Mjumbe
- (xix) Kamishna wa Kazi - Katibu

(b) MAJUKUMU YA KAMATI

- (i) Kushirikiana na Uongozi wa Mkoa ambao sherehe za Siku ya Wafanyakazi zitafanyika kupanga shughuli zitakazofanyika siku ya sherehe.
- (ii) Kuandaa ratiba ya sherehe kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa.
- (iii) Kuhakikisha vifaa vya sherehe vinapatikana
- (iv) Kuhamasisha wafanyakazi wa sekta mbalimbali kupitia vyama vyao vya wafanyakazi kushiriki katika maandamano na sherehe ya siku ya wafanyakazi duniani.
- (v) Kufanya utaratibu wa kumpata mgeni rasmi.
- (vi) Kuandaa mialiko ya watakaohudhuria sherehe.
- (vii) Kuratibu upatikanaji wa wafanyakazi hodari pamoja na zawadi watakazopewa.
- (viii) Kuratibu uandaaji wa mabango na maonyesho ya wafanyakazi siku ya sherehe.
- (ix) Kufanya tathmini baada ya sherehe.

Hatua za Maandalizi

(a) Taarifa

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wote. Taarifa hii pia itapelekwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa. Taarifa itatolewa miezi miwili kabla ya sherehe.

(b) Vikao vya Maandalizi

Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani itapanga idadi ya vikao vya maandalizi ya sherehe kwa kushirikiana na Kamati ya Sherehe ya Mkoa ambapo sherehe zitafanyika.

Kamati ya Maandalizi kwa kushirikiana na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaendesha vikao vitatu.

- (i) Kikao cha kwanza ni cha kupokea taarifa ya Maandalizi ya awali ya sherehe.
- (ii) Kikao cha pili ni cha kufuatilia na kupata taarifa za utekelezaji wa masuala yaliyokubalika katika kikao cha kwanza.
- (iii) Kikao cha tatu ni cha kuona mazoezi kwa vitendo katika uwanja wa sherehe ya Sikukuu ya Wafanyakazi.
- (iv) Kikao cha nne kitakuwa ni kikao cha tathmini ya sherehe na kifanyike ndani ya siku mbili (2) baada ya sherehe.

(c) Ratiba ya Sherehe

Ratiba itazingatia yafuatayo:-

- Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
- Muda
- Matukio
- Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba itaandaliwa mwezi mmoja kabla ya kilele cha maadhimisho na kuwasilishwa kwa mgeni rasmi kwa ajili ya kupitishwa.

(d) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa itaandaliwa mapema ili kuruhusu uandaaji wa kadi na barua za mialiko

(i) Barua za Mialiko

Viongozi wafuatao watapewa barua za mwaliko itakapobidi kuwaalika. Barua za mialiko zitatolewa kwa kushirikisha Idara ya Maadhimisho na sherehe za kitaifa:-

- Viongozi wa Kitaifa (Waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Jaji Mkuu na Spika wa Bunge (waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).

Aidha, makundi tajwa hapo juu iwapo wataalikwa watapewa pia kadi za mialiko isipokuwa Viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

(ii) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitayarishwe kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Kadi za mialiko zitatolewa kwa Viongozi wafuatao:-

- Mawaziri, na Naibu Mawaziri
- Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu
- Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama
- Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea
- Wakurugenzi katika Wizara
- Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi
- Wawakilishi wa Mashirika mbali mbali

(e) Hotuba ya Mgeni Rasmi

- Katika Sherehe hizi rasimu ya hotuba ya Mgeni rasmi itaratibiwa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya Kazi, na kuiwasilisha kwa Mgeni Rasmi mwezi mmoja kabla ya sherehe kwa hatua zaidi.

(f) Vikundi Mbalimbali vya Burudani

- Vikundi vya sanaa na burudani vitapangiwa utaratibu mzuri utakaoandaliwa wa kutumbuiza ili kuepusha migongano na kelele.
- Vikundi hivyo vijulikane na kukaguliwa mapema na Kamati ya Sherehe ya Mkoa, kabla ya kamati iliyoundwa na Wizara yenye dhamana kukagua.

(g) Mapambo

- Kutakuwa na mapambo uwanjani, eneo la Sherehe. Mapambo yatakuwa ya maua na vitambaa. Matumizi ya maputo (balloons) kama sehemu ya mapambo hayataruhusiwa. Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana watagharamia.

(h) Barabara

Ukarabati wa Barabara zitakazotumika kupita viongozi wakati wa sherehe hizi utasimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya barabara (TANROADS), Mkoa/ Jiji sherehe zitakapofanyika.

(i) Jukwaa

Jukwaa la kukaa Viongozi wa Kitaifa ambapo sherehe zitafanyika litaandaliwa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya kazi.

(j) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa itaandaa mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa. Wizara yenye dhamana ya masuala ya kazi itagharamia huduma hii.

(k) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya kuwawezesha wananchi na waalikwa kufuatilia matukio yanavyoendelea. Vipaza sauti katika sherehe hizi vitawekwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa. Wizara yenye dhamana itagharamia huduma hii.

(l) Maji

Kamati ya maandalizi ihakikishe uwepo wa maji ya kutosha kwenye eneo la Sherehe.

(m) Vyoo

Kamati ya maandalizi ihakikishe uwepo wa vyoo safi kwa ajili ya viongozi na wananchi.

(n) Jenereta

Kamati ya maandalizi ihakikishe uwepo wa Jenereta la dharura. Jenereta liwepo uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe.

(o) Huduma ya Kwanza

Daktari wa Mkoa ahakikishe uwepo wa huduma ya kwanza na gari la wagonjwa.

(p) Bendera

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iwapo ndiye atakuwa mgeni rasmi)

(q) Maandamano

- Yataandaliwa maandamano ya Wafanyakazi kutoka sehemu mbalimbali za kazi. Maandamano hayo yatapokelewa na Mgeni Rasmi.

SEHEMU YA TISA

MAONYESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA

Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa (SabaSaba) hufanyika kuanzia tarehe 29 Juni na kufikia kilele tarehe 7 Julai kila mwaka. Maonyesho haya huandaliwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwa kusimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Itifaki ya Viongozi

Sherehe hizi ni za Kitaifa hivyo zitafuata Itifaki zote zinazohusiana na Sherehe za Kitaifa.

KAMATI YA MAANDALIZI

Kutakuwa na Kamati ya Maandalizi ya Wizara yenye dhamana na masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kushirikiana na Mamlaka ya Biashara Tanzania (Tan Trade);

MUUNDO WA KAMATI YA MAANDALIZI

Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) itakuwa na wajumbe wafuatao:-

- Katibu MKuu, Wizara yenye dhamana ya masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko - Mwenyekiti
- Mkurugenzi Mtendaji, Fursa sawa kwa wote - Mjumbe
- Mkurugenzi, Idara ya Uhamiaji - Mjumbe
- Mkurugenzi wa Jiji - Mjumbe

- Mkurugenzi Mtendaji, Baraza la Biashara, Viwanda na Kilimo - Mjumbe
- Katibu Mtendaji, Shirikisho la Viwanda Tanzania - Mjumbe
- Mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa Polisi - Mjumbe
- Afisa Afya Mfawidhi, Manispaa ya Temeke - Mjumbe
- Mkurugenzi Mtendaji, Tanzania Private Sector Foundation - Mjumbe
- Rais wa Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo Zanzibar - Mjumbe
- Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu - Mjumbe
- Kamishna wa Ushuru, Mamlaka ya Mapato Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi wa Kanda wa TANESCO - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Utangazaji Tanzania - Mjumbe
- Mwakilishi Bodi ya Biashara ya Nje Zanzibar - Mjumbe
- Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) - Mjumbe
- Kamishna Mkuu, Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevyva - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Bandari Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi wa Habari (MAELEZO) - Mjumbe
- Mkurugenzi Mtendaji SUMATRA - Mjumbe
- Kamishna Mkuu, Chama cha Skauti Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi Mtendaji, Kituo cha Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar - Mjumbe

- Mkurugenzi Mkuu, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi, Utafiti na Mipango, Mamlaka ya Biashara Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi, Fedha na Utawala, Mamlaka ya Biashara Tanzania - Mjumbe
- Mkurugenzi Mtendaji, Bodi ya Utalii - Mjumbe
- Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu, Idara ya Usalama wa Taifa - Mjumbe
- Mkuu wa Itifaki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mjumbe
- Katibu Tawala, Mkoa wa Dar es Salaam - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Biashara Tanzania - Katibu

MAJUKUMU YA KAMATI YA MAANDALIZI

- (i) Kupanga shughuli zitakazofanyika katika sherehe za Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa.
- (ii) Kuandaa ratiba ya Sikukuu ya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa.
- (iii) Kuandaa na kuendesha vikao vya maandalizi ya Sherehe Maonyesho ya Kibiashara ya Kimataifa.
- (iv) Kuandaa vikundi vya burudani na sanaa vitakavyoshiriki katika sherehe za Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa.
- (v) Kuratibu wafanyabiashara wa Kitaifa na wa Kimataifa watakaoshiriki katika maonyesho ya Biashara katika wiki ya sherehe hizo.
- (vi) Kuratibu ujenzi wa vibanda na maeneo ya maonyesho katika uwanja wa maonyesho.
- (vii) Kuhakikisha usafi, usalama na uhakika wa miundo mbinu katika uwanja wa maonyesho.

- (viii) Kutoa taarifa kwa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa kuhusu hatua mbali mbali za maandalizi.
- (ix) Kufanya tathmini ya Sherehe za Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa na kutoa taarifa kwa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa.

MAANDALIZI YA SHEREHE

Maandalizi ya Sherehe hizi, pamoja na mambo mengine yatahusu mambo yafuatayo:-

(a) Ratiba ya Sherehe

Ratiba izingatie yafuatayo:-

- Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
- Muda
- Matukio
- Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba ikamilike mwezi mmoja kabla ya kilele cha maadhimisho na kuwasilishwa kwa Mgeni rasmi kwa ajili ya kupitishwa.

(b) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa iandaliwe mapema ili kuruhusu uandaaji wa kadi na barua za mialiko.

(i) Barua za Mialiko

Viongozi wafuatao watapewa barua za mwaliko itakapobidi kuwaalika.

- Viongozi wa Kitaifa (Waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Jaji Mkuu na Spika wa Bunge (waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).

Aidha, makundi tajwa hapo juu watapewa pia kadi za mialiko isipokuwa Viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

(ii) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitayarishwe kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Kadi za mialiko zitolewe kwa Viongozi wafuatao:-

- Mawaziri na Naibu Mawaziri
- Makatibu Wakuu wa Naibu Makatibu Wakuu
- Mabalazi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,
- Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea
- Wakurugenzi katika Wizara za Serikali

(c) Hotuba ya Mgeni Rasmi

Rasimu ya hotuba ya Mgeni rasmi itaandaliwa na kuratibiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko na kuiwasilisha kwa Mgeni Rasmi mwezi mmoja kabla ya Sherehe kwa ajili ya hatua zaidi.

(d) Vikundi

Vikundi vya sanaa na burudani vitawekewa utaratibu mzuri wa kutumbuiza ili kuepusha migongano na kelele. Vikundi hivyo vitakaguliwa mapema na Kamati ya maandalizi ya Sherehe hiyo.

(e) Mapambo

Kutakuwa na mapambo eneo la Sherehe/tukio. mapambo yatakuwa ya maua. Matumizi ya maputo (balloons) kama sehemu ya mapambo hayataruhusiwa. Wizara

yenye dhamana ya masuala ya Viwanda na Biashara itagharamia.

(f) Barabara

Ukarabati wa Barabara zitakazotumika kupita viongozi wakati wa sherehe hizi utasimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya barabara (TANROADS) na Mkoa/Jiji sherehe zitakapofanyika.

(g) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya wananchi kufuatilia matukio.

Vipaza sauti katika sherehe hizi vitawekwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Wizara yenye dhamana na masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko kupitia Mamlaka ya Biashara Tanzania itagharamia huduma hii.

(h) Jukwaa la Kukaa Viongozi

Jukwaa la kukaa Viongozi litaandaliwa na Mamlaka ya Biashara Tanzania.

(i) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaaandaa Mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa. Wizara yenye dhamana ya masuala ya Viwanda na Biashara itagharamia huduma hii.

(j) Jenereta

Liwepo Jenereta uwanjani kwa ajili ya dharura ya umeme juma moja (1) kabla ya sherehe.

(k) Maji

Yawepo maji ya kutosha kwenye eneo la tukio/sherehe

(l) Vyoo

Uwepo uhakika wa vyoo visafi kwa ajili ya Viongozi na Wananchi.

(m) Bendera

Bendera zitakazotundikwa eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa.
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Bendera ya Nchi ambayo mgeni rasmi atatoka.

SEHEMU YA KUMI

SIKUKUU YA WAKULIMA (NANENANE)

Sherehe za Wakulima (Nanenane) zitafanyika kuanzia tarehe 01 hadi tarehe 8 Agosti kila mwaka. Kilele cha Sherehe hizo ni tarehe 8 Agosti. Sherehe zitafanyika Kitaifa sehemu ambayo itaelekezwa na Kamati ya Maandalizi chini ya usimamizi na uratibu wa Wizara yenye dhamana na masuala ya kilimo.

Sherehe hizi ni za Kitaifa hivyo zitafuata itifaki zote zinazohusiana na Sherehe za Kitaifa. Wizara yenye dhamana na masuala ya kilimo itaandaa kwa kuwashirikisha Wadau muhimu katika kufanikisha sherehe hizi.

KAMATI YA MAANDALIZI

(a) Muundo wa Kamati

Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za Sikukuu ya Wakulima itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

- (i) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana - Mwenyekiti
na Kilimo
- (ii) Mkurugenzi, Idara ya Utafiti na Mafunzo - Mjumbe
ya Kilimo
- (iii) Mkurugenzi, Idara ya Umwagiliaji na - Mjumbe
Huduma za Ufundi
- (iv) Mkurugenzi, Idara ya Usalama na - Mjumbe
Chakula
- (v) Mkurugenzi, Idara ya Matumizi Bora ya - Mjumbe
Ardhi
- (vi) Mkurugenzi, Idara ya Ushirika - Mjumbe
- (vii) Mkurugenzi, Idara ya Masoko - Mjumbe

- (viii) Mkurugenzi, Idara ya Maadhimisho - Mjumbe
na Sherehe za Taifa
- (ix) Mwakilishi kutoka Idara ya Usalama - Mjumbe
wa Taifa
- (x) Mkuu wa Itifaki - Mjumbe
- (xi) Afisa Habari wa Wizara husika - Mjumbe
- (xii) Mwenyekiti wa TASO Taifa - Mjumbe

(b) Vikao vya Maandalizi

Wizara yenye thamana na masuala ya Kilimo itapanga idadi ya vikao vya maandalizi ya sherehe kwa kushirikiana na Kamati ya sherehe ya Mkoa ambako Sherehe zitafanyika. Kamati ya Maandalizi ya Wizara itaendesha vikao visivyozidi vinne vya maandalizi.

- (i) Kikao cha kwanza ni cha kupokea taarifa ya maandalizi ya awali ya sherehe kutoka kwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Kilimo.
- (ii) Kikao cha pili ni kufuatilia na kupata taarifa za utekelezaji wa masuala yaliyokubalika katika kikao cha kwanza.
- (iii) Kikao cha tatu ni cha kuona mazoezi kwa vitendo katika uwanja wa maonyesho ya sikukuu ya wakulima.
- (iv) Kikao cha nne ni cha tathmini kifanyike ndani ya wiki mbili baada ya sherehe.

(c) Ratiba ya Sherehe

Ratiba izingatie yafuatayo:-

- Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
- Muda
- Matukio
- Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba ikamilike mwezi mmoja kabla ya kilele cha maadhimisho na kuwasilishwa kwa Mgeni rasmi kwa ajili ya kupitishwa.

(d) Barua na Kadi za Mialiko

Orodha ya waalikwa itaandaliwa mapema ili kuruhusu uandaaji wa kadi na barua za mialiko

(i) Barua za Mialiko

Viongozi wafuatao watapewa barua za mwaliko itakapobidi kuwaalika.

- Viongozi wa Kitaifa (Waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Jaji Mkuu na Spika wa Bunge (waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Viongozi wa Vyama vya Siasa ngazi ya Taifa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu)
- Katibu Mkuu Kiongozi

Aidha, makundi tajwa hapo juu iwapo wataalikwa watapewa pia kadi za mialiko isipokuwa Viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

(ii) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitayarishwe kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Kadi zitatolewa kwa Viongozi wafuatao:-

- Mawaziri na Naibu Mawaziri
- Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu
- Mabalози na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama
- Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea
- Wakurugenzi katika Wizara za Serikali

(e) Hotuba ya Mgeni Rasmi

Katika Sherehe hizi rasimu ya hotuba ya Mgeni rasmi itaandaliwa na Wizara yenye dhamana ya Kilimo kuiwasilisha kwa Mgeni Rasmi mwezi mmoja kabla ya sherehe.

(f) Vikundi Mbalimbali vya Burudani

Vikundi vya sanaa na burudani vipangiwe utaratibu mzuri wa kutumbuiza ili kuepusha migongano na kelele. Vikundi hivyo vijulikane na kukaguliwa mapema na Kamati ya Sherehe ya Mkoa kabla ya kukaguliwa na kamati ya Wizara yenye dhamana.

(g) Mapambo

Kutakuwa na mapambo katika eneo la Sherehe. Mapambo yatakuwa ya maua. Matumizi ya maputo (balloons) kama sehemu ya mapambo hayataruhusiwa. Wizara yenye dhamana ya Kilimo itagharamia.

- Usafi wa Mkoa/Jiji na barabara utasimamiwa na uongozi wa Mkoa na Jiji.

(h) Ukarabati wa Barabara

Ukarabati wa Barabara zitakazotumika kupita viongozi wakati wa sherehe hizi utasimamiwa na Wizara yenye dhamana ya barabara (TANROADS), na Mkoa au Jiji Sherehe zitakapofanyika.

(i) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kufuatilia matukio. Vipaza sauti katika sherehe hizi vitawekwa na Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Wizara yenye dhamana na masuala ya Kilimo itagharamia huduma hii.

(j) Jukwaa la Kukaa Viongozi

Jukwaa la kukaa Viongozi wa Kitaifa ambapo sherehe zitafanyika litatakiwa kuwa imara na zuri.

(k) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa itaaandaa Mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa. Wizara yenye dhamana na Kilimo itagharamia huduma hii.

(l) Jenereta

Kamati ya maandalizi ihakikishe uwepo wa Jenereta uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe.

(m) Maji

Kamati ya maandalizi ihakikishe uwepo na maji ya kutosha kwenye eneo la tukio/sherehe.

(n) Huduma ya Kwanza

Daktari wa Mkoa sherehe zinapofanyika ahakikishe uwepo wa huduma ya kwanza na gari la wagonjwa.

(o) Vyoo

Viwepo vyoo visafi kwa ajili ya matumizi ya viongozi na wananchi.

(p) Bendera:

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa.
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo ndiye mgeni rasmi.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE NA KILELE CHA MBIO ZA MWENGE

Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere huadhimishwa tarehe 14 Oktoba ya kila mwaka. Maadhimisho haya huandaliwa na kuratibiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya vijana.

Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere yanaenda sambamba na wiki ya Vijana ambayo inafikia Kilele cha Mbio za Mwenge. Serehe hizi ni za Kitaifa hivyo Itifaki zote zinazohusiana na Serehe za Kitaifa zitafuatwa. Wizara yenye dhamana na Vijana itaandaa kwa kuwashirikisha Wadau muhimu katika kufanikisha serehe hii.

KAMATI YA MAANDALIZI

(a) Muundo wa Kamati

Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itakuwa na wajumbe wafuatao:-

- | | | |
|--------|---|--------------|
| (i) | Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana na masuala ya Vijana | - Mwenyekiti |
| (ii) | Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma | - Mjumbe |
| (iii) | Mkurugenzi wa Sera na Mipango | - Mjumbe |
| (iv) | Kamishna wa Kazi | - Mjumbe |
| (v) | Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi | - Mjumbe |
| (vi) | Mkurugenzi wa Maadhimisho na Serehe za Taifa | - Mjumbe |
| (vii) | Mkuu wa Itifaki | - Mjumbe |
| (viii) | Mwakilishi Idara ya Usalama wa Taifa | - Mjumbe |

- (ix) Mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa Polisi - Mjumbe
- (x) Katibu Tawala wa Mkoa Sherehe za kilele cha mbio za Mwenge zitakapofanyika - Mjumbe
- (xi) Katibu Tawala wa Mkoa Mwenge utakapowashwa. - Mjumbe
- (xii) Afisa Maendeleo ya Vijana, Mwenge utakapowashwa na sherehe za kilele cha mbio za mwenge zitakapofanyika. - Mjumbe
- (xiii) Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana Sherehe za kilele cha mbio za mwenge zitakapofanyika. - Katibu

(b) Majukumu ya Kamati

- (i) Kuandaa ratiba za sherehe za Uwashaji na kilele cha mbio za Mwenge (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere).
- (ii) Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kupendekeza majina ya vijana watakaokimbiza Mwenge Kitaifa.
- (iii) Kupendekeza **kaulimbiu** ya Mwenge katika mwaka husika.
- (iv) Kushirikiana na Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa kuhusu upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya sherehe.
- (v) Kuandaa mialiko ya watakaohudhuria sherehe.
- (vi) Kuratibu uandaaji wa hotuba za wageni rasmi kwenye sherehe za Uwashaji na kilele cha mbio za Mwenge (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere).
- (vii) Kuandaa tafrija.
- (viii) Kufanya tathmini ya Maadhimisho.

HATUA ZA MAANDALIZI

Kamati ya Maandalizi ya Sherehe hizi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuandaa yafuatayo:-

(a) Taarifa

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wote miezi miwili kabla ya sherehe. Taarifa hii pia itapelekwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa.

(b) Vikao vya Maandalizi

Wizara yenye dhamana na maendeleo ya vijana itapanga idadi ya vikao vya maandalizi kwa kushirikiana na Kamati za Sherehe za Mikoa ambayo sherehe za Uwashaji wa Mwenge na Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere vitafanyika.

Kamati ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa kwa kushirikiana na Kamati ya Maandalizi ya Sherehe ya Wizara itaendesha vikao visivyopungua vitano.

- (i) Kikao cha kwanza ni cha kupokea taarifa ya maandalizi ya awali kutoka wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana.
- (ii) Kikao cha pili ni cha kupata taarifa ya utekelezaji wa masuala yaliyokubalika katika kikao cha kwanza.
- (iii) Kikao cha tatu kuona mazoezi kwa vitendo katika Uwanja wa Maadhimisho ya Mwalimu Nyerere na kilele cha Mbio za Mwenge.
- (iv) Kikao cha nne ni cha tathmini ya sherehe kwa ajili ya kupata taarifa ya utekelezaji wa kilele cha mbio za Mwenge na Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Kikao hiki kifanyike ndani ya wiki mbili baada ya sherehe.

- (v) Kikao cha tano ni kikao cha tathmini ya
- Sherehe ya Kuwasha Mwenge
 - Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere/Kilele cha Mbio za Mwenge.

(c) Ratiba ya Sherehe

Ratiba izingatie yafuatayo:-

- Jina na mahali sherehe zitakapofanyika
- Muda
- Matukio
- Wahusika

Aidha, rasimu ya ratiba ikamilike mwezi mmoja kabla ya kilele cha maadhimisho na kuwasilishwa kwa Mgeni rasmi kwa ajili ya kupitishwa.

(d) Kadi na Barua za Mialiko

Orodha ya waalikwa iandaliwe mapema ili kuruhusu uandaaji wa kadi na barua za mialiko.

(i) Kadi za Mialiko

Kadi za mialiko zitayarishwe kwa kuzingatia orodha ya waalikwa. Mialiko itatolewa kwa Viongozi wafuatao:-

- Mawaziri,
- Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa
- Makatibu Wakuu
- Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama
- Wakuu wa Taasisi na Idara zinazojitegemea
- Wakurugenzi katika Wizara za Serikali

(ii) Barua za Mialiko

Viongozi wafuatao watapewa barua za mwaliko itakapobidi kuwaalika

- Viongozi wa Kitaifa (Waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Jaji Mkuu na Spika wa Bunge (waliopo Madarakani na Wastaafu).
- Viongozi wa Vyama vya Siasa (Wenyeviti na Makatibu Wakuu).

Aidha, makundi tajwa hapo juu watapewa pia kadi za mialiko isipokuwa Viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani na wastaafu.

(e) Hotuba ya Mgeni Rasmi

Katika Sherehe hizi rasimu ya hotuba ya Mgeni rasmi itaandaliwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya vijana na kuiwasilisha kwa Mgeni Rasmi mwezi mmoja kabla ya Sherehe.

(f) Vikundi Mbalimbali vya Burudani

Vikundi vya sanaa na burudani vipangiwe utaratibu mzuri wa kutumbuiza ili kuepusha migongano na kelele. Vikundi hivyo vijulikane na kukaguliwa mapema na Kamati ya Sherehe ya Mkoa.

(g) Mapambo

Kutakuwa na mapambo uwanjani, eneo la Sherehe. Mapambo yatakuwa ya maua, vitambaa n.k. Matumizi ya maputo (balloons) kama sehemu ya mapambo hayataruhusiwa. Wizara yenye dhamana na masuala ya vijana watagharamia.

(h) Ukarabati wa Barabara

Ukarabati wa Barabara zitakazotumika kupita viongozi wakati wa sherehe hizi utasimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya barabara.

(i) Vipaza Sauti

Kutakuwa na vipaza sauti ndani na nje ya uwanja kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kusikia. Vipaza sauti katika sherehe hizi vitawekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa), Wizara yenye dhamana na masuala ya vijana itagharamia uwekaji wa Vipaza Sauti.

(j) Jukwaa

Jukwaa la kukaa Viongozi wa Kitaifa ambapo sherehe zitafanyika litatakiwa kuwa imara na zuri. Litaandaliwa na Kamati ya Maandalizi ya Sherehe.

(k) Mazulia Mekundu

Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa itaandaa Mazulia mekundu kwa ajili ya sehemu watakapopita na kukaa Viongozi wa Kitaifa. Wizara yenye dhamana itagharamia huduma hii.

(l) Jenereta

Liwepo Jenereta uwanjani kwa ajili ya dharura ya umeme liwepo uwanjani juma moja (1) kabla ya sherehe.

(m) Maji

Pawepo maji ya kutosha kwenye eneo la sherehe

(n) Vyoo

Kuwepo na vyoo visafi kwa ajili ya Viongozi na wananchi.

(o) Huduma ya Kwanza

Wizara yenye dhamana itahakikisha uwepo wa huduma ya kwanza na gari la wagonjwa.

(p) Bendera

Bendera zitakazopandishwa katika eneo la sherehe ni:-

- Bendera ya Taifa.
- Bendera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bendera ya nchi ambayo mgeni Rasmi atatoka.

SURA YA TATU

MISIBA YA VIONGOZI WA KITAIFA NA VIONGOZI WENGINE

Sura hii inaweka utaratibu wa kudumu wa mazishi kwa Viongozi wa Kitaifa walioko madarakani na waliostaafu kwa Mujibu wa Sheria Na. 1 ya Mwaka 2006 inayohusu mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu unaainisha Viongozi wanaostahili mazishi ya kitaifa, aina ya mazishi, kutangaza msiba wa kitaifa, majukumu ya Kamati iliyoundwa kisheria kusimamia misiba, maeneo ya mazishi ya Viongozi, kutoa heshima za mwisho, gwaride, matumizi ya alama ya msiba, upatikanaji wa fedha za mazishi na mialiko ya viongozi wa nchi za nje watakaoshiriki kwenye mazishi.

SEHEMU YA KWANZA

VIONGOZI AMBAO MISIBA YAO NI YA KITAIFA

Kwa mujibu wa Sheria Na.1 ya mwaka 2006, Viongozi ambao wanapofariki misiba yao ni ya kitaifa ni wafuatao:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Makamu wa Rais
- Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Waziri Mkuu
- Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Jaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar
- Viongozi wote waliotajwa hapo juu wastaafu.
- Waziri Kiongozi Mstaafu

SEHEMU YA PILI
KAMATI ZA MAZISHI YA VIONGOZI WA
KITAIFA

Kutakuwa na Kamati mbili za Kitaifa zitakayosimamia na kuratibu mazishi ya viongozi wa Kitaifa. Muundo wa majukumu ya Kamati hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) KAMATI KUU YA MAZISHI YA VIONGOZI
WA KITAIFA

- | | | | |
|--------|---|---|----------------------|
| (i) | Waziri Mkuu | - | Mwenyekiti |
| (ii) | Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar | - | Makamu
Mwenyekiti |
| (iii) | Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma | - | Mjumbe |
| (iv) | Katibu Mkuu Kiongozi | - | Mjumbe |
| (v) | Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | - | Mjumbe |
| (vi) | Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | - | Mjumbe |
| (vii) | Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi | - | Mjumbe |
| (viii) | Waziri wa Fedha | - | Mjumbe |
| (ix) | Waziri wa Fedha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar | - | Mjumbe |
| (x) | Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) | - | Mjumbe |
| (xi) | Waziri wa Miundombinu | - | Mjumbe |

(xii)	Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar	-	Mjumbe
(xiii)	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Zanzibar	-	Mjumbe
(xiv)	Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii	-	Mjumbe
(xv)	Mwanasheria Mkuu wa Serikali	-	Mjumbe
(xvi)	Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu	-	Katibu

Waalikwa

Viongozi wafuatao wanaweza kualikwa

- (i) Katibu Mkuu Ikulu
- (ii) Mkuu wa Majeshi
- (iii) Inspekta Jenerali wa Polisi
- (iv) Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa
- (v) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

MAJUKUMU YA KAMATI

Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia maandalizi ya mazishi ya viongozi wa kitaifa.
- Kutoa taarifa juu ya maendeleo ya maandalizi ya shughuli za mazishi.
- Kupitisha makadirio ya Bajeti ya gharama za mazishi.
- Kupokea maelekezo kutoka kwenye mamlaka na kuyaelekeza kwenye Kamati ya utendaji.
- Kushauri na kuelekeza Kamati ya utendaji kuhusiana na utekelezaji wa shughuli zote za mazishi.
- Kupokea na kujadili mapendekezo yatakayoandaliwa na Kamati ya utendaji.
- Kupitia na kutoa maamuzi kutokana na taarifa ya mazishi kama itakavyowasilishwa na Kamati ya utendaji.
- Kutekeleza majukumu yahasuyo mazishi kama itakavyoona inafaa.

(b) KAMATI YA UTENDAJI

Kamati ya Utendaji ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i)	Katibu Mkuu Kiongozi	Ofisi ya Rais,Ikulu	Mwenyekiti
(ii)	Katibu Mkuu	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	Mjumbe
(iii)	Katibu Mkuu	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	Mjumbe
(iv)	Katibu Mkuu	Wizara ya Mambo ya Ndani	Mjumbe
(v)	Katibu Mkuu	Wizara ya Fedha na Uchumi	Mjumbe
(vi)	Katibu Mkuu	Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar	Mjumbe
(vii)	Katibu Mkuu	Wizara ya Miundombinu	Mjumbe
(viii)	Katibu Mkuu	Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)	Mjumbe
(ix)	Katibu Mkuu	Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar	Mjumbe
(x)	Katibu Mkuu	Baraza la Mapinduzi Zanzibar	Mjumbe
(xi)	Katibu Mkuu	Ofisi ya Waziri Mkuu	Katibu

Waalikwa

Viongozi wafuatao wanaweza kualikwa

- (i) Katibu Mkuu Ikulu
- (ii) Mkuu wa Majeshi
- (iii) Inspekta Jenerali
- (iv) Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa

MAJUKUMU YA KAMATI YA UTENDAJI

Majukumu ya Kamati ya Utendaji yatakuwa:-

- Kuandaa bajeti ya gharama za mazishi na kuiwasilisha kwenye Kamati ya mazishi ya kitaifa kwa ajili ya kupitishwa.
- Kuratibu mipango yote ya mazishi na kusimamia shughuli zote kama itakavyoelekezwa na Kamati ya mazishi ya kitaifa ili kutoa muelekeo wa utendaji.
- Kutoa maelekezo ya utendaji wa shughuli zote za mazishi kwa watendaji na kamati ndogo zitakazohusishwa na kuteuliwa na Mwenyekiti wa Kamati.
- Kuandaa ratiba ya shughuli za mazishi na kuiwasilisha kwenye Kamati ya kitaifa.
- Kutoa taarifa kwa kamati ya mazishi ya kitaifa juu ya maandalizi ya shughuli za mazishi.
- Kuandaa taarifa ya shughuli za mazishi na kuiwasilisha kwenye Kamati ya mazishi ya kitaifa.
- Kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na kamati ya mazishi ya kitaifa.
- Kuandaa Mialiko.
 - Kamati ya Mazishi ya Viongozi wa kitaifa itapendekeza na kuamua watu au Taasisi zitakazoshiriki kwenye shughuli za mazishi ya Viongozi wa Kitaifa.
 - Kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 25 cha Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa (The National Leaders Funerals Act No. 1 of 2006), Wajumbe wa Kamati ya mazishi ya Viongozi wa Kitaifa na Kamati ya Utendaji wanatakiwa kutunza siri za masuala yote yahasuyo taarifa na mwenendo wa msiba kama vile matangazo ya vifo na taratibu za mazishi ya Viongozi wa Kitaifa isipokuwa kwa idhini ya mamlaka husika.
 - Mwenyekiti wa Kamati ya mazishi ya Viongozi wa Kitaifa anaweza kumruhusu mjumbe yeyote wa Kamati kutoa taarifa kwa Umma au kwa kikundi maalum cha Watu endapo kutakuwa na umuhimu wa kutoa taarifa hiyo au kama taarifa za mwenendo wa shughuli za mazishi utahitajika kuufikia Umma.

SEHEMU YA TATU

MAENEO YA KUZIKIA NA AINA ZA MAZISHI

(a) ENEO LA KUZIKIA VIONGOZI WA KITAIFA

Eneo la Mji Mpya kwenye Vilima vya Iyumbu katika Manispaa ya Dodoma limetengwa kwa ajili ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa. Eneo hili litasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na litatumika kwa ajili ya mazishi pamoja na shughuli zote zinazoambatana na mazishi.

Aidha, kutakuwa na Makaburi ya Kitaifa katika Mikoa ambako Mashujaa, Viongozi na Watu mashuhuri ambao wametoa mchango mkubwa kwa Taifa watazikuwa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa na mamlaka ya mwisho na uwezo wa kumtangaza mtu yeyote kuwa Shujaa au Mashuhuri ili azikwe kwenye eneo maalum katika ngazi ya mkoa.

(b) USIMAMIZI WA MAENEO YA MAKABURI YA VIONGOZI

Maeneo ya Makaburi ya Viongozi yatasimamiwa na Idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Majukumu ya Idara hiyo yatakuwa yafuatayo:-

- Kusimamia na kuratibu maeneo ya makaburi ya kitaifa.
- Kutunza kumbukumbu za mashujaa (Gallery).
- Kuandaa maonyesho ya kumbukumbu za mashujaa.
- Kufanya utafiti wa masuala ya urithi wa Taifa kuhusiana na harakati mbalimbali za ukombozi.
- Kutunza na kuratibu kumbukumbu za Waasisi wa Taifa.
- Kufuatilia na kukusanya vifaa mbalimbali vilivyotumika katika mazishi ya kiongozi wa Kitaifa kwa ajili ya kuhifadhi kama kumbukumbu.

(c) AINA ZA MAZISHI

Kutakuwa na aina mbili za mazishi ya Viongozi wa Kitaifa ambayo ni:

(i) Mazishi ya Kitaifa (State Funerals)

Mazishi ya kitaifa yatamhusu Kiongozi wa Kitaifa ambaye amewahi kushika wadhifa wa Urais.

(ii) Mazishi ya Kiserikali (Government Funeral)

Mazishi ya Kiserikali yatawahusu viongozi wa kitaifa ambao wanaitumikia au wameitumikia Serikali kama Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Jaji Mkuu na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA NNE

MAZISHI

(a) UTARATIBU WA KUFUATWA UNAPOTOKEA MSIBA WA KITAIFA

Kutakuwa na taratibu za kutangaza misiba ya kitaifa kama ilivyoainishwa hapa chini:

- (i) Endapo msiba wa kiongozi wa kitaifa (National Leader) au kiongozi aliyebainishwa kwa mujibu wa Sheria hii ambaye ni Spika au Jaji Mkuu (*Specified Leader*) utatokea, Rais atatangaza kutokea kwa msiba huo.
- (ii) Rais atatangaza kifo cha kiongozi wa kitaifa mara baada ya kupokea taarifa na uthibitisho kutoka kwa daktari juu ya kutokea msiba huo. Taarifa hiyo itataja tarehe, muda na sababu za kifo.
- (iii) Endapo msiba wa kiongozi wa kitaifa au kiongozi maalum utatokea Rais anapokuwa safarini au anapokuwa hayupo Ofisini, Kiongozi anayekaimu madaraka ya Urais atakuwa na jukumu la kutangaza kifo cha Kiongozi wa Kitaifa.
- (iv) Ataitisha mkutano wa Baraza la Mawaziri na kutangaza:-
 - Endapo msiba utakuwa wa Rais Mstaafu basi kutakuwa na maombolezo ya siku saba (7) na Bendera kupepea nusu mlingoti.
 - Endapo msiba utakuwa wa Makamu wa Rais aliyepo madarakani, kutakuwa na siku kumi na nne (14) za maombolezo ya kitaifa na Bendera kupepea nusu mlingoti.

- Endapo msiba utakuwa wa Makamu wa Rais Mstaafu, kutakuwa na siku saba (7) za maombolezo ya kitaifa na Bendera kupepea nusu mlingoti.
 - Endapo msiba utakuwa wa Waziri Mkuu aliyepo madarakani kutakuwa na maombolezo ya siku saba (7) za maombolezo ya kitaifa na Bendera kupepea nusu mlingoti.
 - Endapo msiba utakuwa wa Waziri Mkuu Mstaafu kutakuwa na siku tano (5) za maombolezo ya kitaifa na Bendera kupepea nusu mlingoti.
- (v) Endapo Rais aliyepo madarakani atafariki Makamu wa Rais atatangaza kutokea kifo cha Rais. Aidha atatangaza siku 21 za maombolezo na Bendera kupepea nusu mlingoti.
- (vi) Endapo kiongozi wa kiserikali atafariki na Rais kupokea taarifa kutoka kwa ndugu wa marehemu atatangaza kifo kupitia vyombo vya habari. Hapatakuwa na siku za maombolezo wala Bendera kupepea nusu mlingoti.
- (vii) Mazishi ya Kiongozi ambaye msiba wake ni wa kitaifa utazingatia misingi na taratibu za dini, mila na desturi ya marehemu kufuatana na sababu za kifo kama Kamati itakavyoona inafaa.
- (viii) Endapo mwili wa marehemu hautapatikana/ kupotea kutokana na sababu za kifo kama vile ajali ya ndege, shughuli za maombolezo zitifanywa kwa kuzingatia misingi ya dini na mila kama itakavyoonekana inafaa.

- (ix) Endapo kifo cha marehemu kimetokana na ugonjwa ambao mazishi yake yanahitaji kuzingatia ushauri wa kitaalam wa Daktari, mamlaka haina budi kuzingatia ushauri huo.

(b) HESHIMA ZA MWISHO

- (i) Mwili wa marehemu utawekwa kwenye Uwanja wa maombolezo kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho au mahali pengine kama Kamati ya mazishi ya kitaifa itakavyoona inafaa. Aidha, vyombo vya Ulinzi na Usalama vitasimamia shughuli zote za kuusafirisha mwili wa marehemu.
- (ii) Muda wa kutoa heshima za mwisho kwa kiongozi wa Kitaifa utaamuliwa na Kamati ya mazishi ya kitaifa kwa kushirikiana na familia ya marehemu au kiongozi wa dini ya marehemu anayehusika.
- (iii) Mwili wa marehemu utachukuliwa na kupelekwa mahali itakapofanyika ibada kulingana na imani ya marehemu au mahali patakapoamuliwa na Kamati ya mazishi kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya ibada na taratibu nyingine za mazishi.
- (iv) Heshima za mwisho kwa Kiongozi wa Serikali zitatolewa mahali patakapoamuliwa na Kamati ya mazishi ya kitaifa kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya ibada na taratibu nyingine za mazishi.

(c) GWARIDE LA MAZISHI

- (i) Kutakuwa na Gwaride maalum litakaloandaliwa na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania kwenye eneo la mazishi kwa kushirikiana na Kamati ya Mazishi ya Kitaifa.

- (ii) Mazishi ya Rais aliyekuwa madarakani au Rais Mstaafu yatahusisha gwaride litakaloandaliwa na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania likiwa na gadi moja iliyokamilika (full guard) na kupigwa Wimbo wa Taifa.
- (iii) Mizinga 21 itapigwa wakati wa mazishi karibu na eneo la makaburi.
- (iv) Jeneza lenye mwili wa marehemu ambaye alikuwa Kiongozi wa Kitaifa au Kiongozi wa Serikali litafunikwa Bendera ya Taifa.
- (v) Bendera iliyotumika kufunika Jeneza lenye mwili wa marehemu aliyekuwa Rais au Rais Mstaafu baada ya mazishi itakabidhiwa kwa familia ya marehemu.
- (vi) Katika mazishi ya Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, Gwaride la mazishi litaandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambalo ni nusu gadi (half guard).

(d) MAHITAJI

- Eneo la mazishi.
- Mahali maalum pa kuhifadhia mwili wa marehemu.
- Mahali pa kutolea heshima za mwisho.
- Eneo la kutunzia vifaa vihusikanavyo na msiba.
- lama za utambulisho wa msiba wa kitaifa (Kupandisha Bendera nusu mlingoti, Vazi la maombolezo).
- Mahali pa kuweka kitabu, Kalamu na picha ya marehemu kwa ajili ya rambirambi.

- Uwanja wa maombolezo.
- Mahema ya ukubwa mbalimbali
- Eneo la kuegesha magari
- Vifaa vya mazishi-Vazi rasmi la marehemu kama lipo, Jeneza, Sanda, Mashada, Bendera ya Serikali, Gari maalum la kubeba mwili wa marehemu (Gun carriage vehicle), Vifaa vya kushushia jeneza kaburini.
- Gari la kubeba wagonjwa (Ambulance)
- Gwaride.
- Muundo wa Kaburi.
- Miundombinu muhimu eneo la mazishi/ maombolezo kama vile Umeme, Maji n.k.
- Jukwaa la kuwekea jeneza
- Vyoo vinavyohamishika.

(e) FEDHA

- Fedha kwa ajili ya kufanikisha shughuli za mazishi ya Viongozi wa Kitaifa zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated fund).
- Fedha hizi zitatumika kugharamia shughuli zifuatazo:-
 - Kuandaa kumbukumbu za Kiongozi aliyefariki.
 - Mahitaji muhimu ya mazishi ya Kiongozi wa Kitaifa au Kiongozi wa Serikali aliyefariki.
 - Kusafirisha mwili wa marehemu Kiongozi wa Kitaifa au Kiongozi wa Serikali na watu wengine wanaohusika na msiba huo.
 - Kulipia gharama zote zitakazotokana na majukumu ya Kamati ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa pamoja na Kamati ya Utendaji ya mazishi ya Viongozi wa Kitaifa.
 - Kulipia gharama zozote za mazishi kama itakavyoelekezwa na Kamati ya mazishi ya Viongozi wa Kitaifa.

